
SportPesa
TZS. 1,065,872,000
BET LEO UWE BILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#



**Lowassa** apewa tuzo kimataifa, familia yanena

UKURASA 3



**IBRAHIMOVIC AHOFIA KUSTAAFU SOKA**

UKURASA 22


# Nipashe

Alhamisi Machi 24, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580894

www.ippmedia.com

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710 LIKE & FOLLOW US


# Samia aibua fursa sekta binafsi

UKURASA 2




Rais Samia Suluhu Hassan akiwa na Waziri wa Ujenzi, Prof. Makame Mbarawa (kushoto), baada ya kuzindua mradi wa nyumba 644, zilizojengwa na serikali kupitia Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), Magomeni Kota mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## YALIYOMO

UKURASA WA 7

**TCB YAZINDUA KADI MALIPO KIMATAIFA**

BENKI ya Biashara Tanzania (TCB) jana imezindua kadi ya malipo ya kidijitali...

## Waziri awatoa hofu wananchi kirusi kipya corona

UKURASA 3



Makamu wa Rais na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya VISA Afrika Mashariki, Corine Nana (kulia) na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Biashara Tanzania (TCB), Sabasaba Moshingi, wakibonyeza kitufe kuzindua rasmi kadi ya Popote Visa, iliyozinduliwa na TCB, jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya kuwarahisishia wateja kupata huduma yoyote mahali popote ndani na nje ya nchi. **PICHA:MPIGAPICHA WETU**

# LHRC na LEAT waja na hoja 12 uchafuzi Mto Mara

• **Imo** vigogo NEMC kuwajibishwa, ACT - Wazalendo yatia neno...

*Endelea ukurasa 2*

**MICHEZO** GEITA GOLD HAKUNA KUPUMZIKA UK.23 | **MAONI, KATUNI** UK.6




Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Wanasheria wa Mazingira kwa Vitendo (LEAT), Dk. Rugemeleza Nshala, akizungumza na waandishi wa habari, Dar es Salaam jana, wakati akitoa tamko la chama hicho, kuhusu uchafuzi wa maji Mto Mara. Kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga. **PICHA: SABATO KASIKA**

# LHRC na LEAT waja na hoja 12 uchafuzi Mto Mara

**Na Mwandishi Wetu**

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) na Chama cha Wanasheria wa Mazingira kwa Vitendo (LEAT) wamependekeza mambo 12 kuhusu uchafuzi wa Mto Mara.

Mwanzoni mwa mwezi huu kuliripotiwa uchafuzi wa maji ya Mto Mara uliosababisha samaki kufa na kuelea huku wakazi wa maeneo jirani wakipata madhara kiafya baada ya kula samaki hao. Akizungumza na waandishi wa habari mkoani Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Anna Henga, alisema kituo hicho kwa kushirikiana na LEAT, walifuatilia kwa lengo la kujiridhisha kuhusu taarifa hizo, wakitembelea baadhi ya vijiji na vitongoji vilivyoathiriwa na uchafuzi huo.

Aliyataja maeneo ambayo maofisa wao waliyatembelea kati ya Machi 17 na 20, mwaka huu kuwa ni pamoja na Makora, Burongo, Bisarwi Kati na Kwikoma yaliyoko Kata ya Manga wilayani Tarime. Anna alisema katika ziara yao kwenye maeneo hayo ya waathirika wa uchafuzi huo, walibaini kuwapo taarifa za vifo vya mifugo ya wakazi wa maeneo hayo vinavyotokana na kunywa maji ya Bonde la Mto Mara yanayopita kwenye vijiji hivyo.

"Tulibaini kuwa katika kipindi cha kati ya mwaka 2018 na 2022, zaidi ya mifugo 800 ilikufa kutokana na kunywa maji yanayodhaniwa kuwa na sumu yanayopita katika Bonde la Mto Mara.

"Katika kipindi cha kati ya Machi mosi na 15 mwaka huu, ng'ombe waliripotiwa kufa kutokana na kunywa maji ya mto huo. Taarifa hizo zilibainisha kuwa mifugo hukonda mithili ya kunyauka hatimaye kufa. "Pale wakazi hao wanapochinja ng'ombe hao baada ya vifo hivyo, imethibitishwa na wenyeji kwamba nyama ilibadilika rangi na kuwa nyeusi, hivyo kutofaa kwa matumizi yoyote ya binadamu. "Pia mwaka 2020 na 2021 kulikuwapo na matukio ya kujirudia kwa wakazi wa vijiji hivyo kukumbwa na ugonjwa wa ngozi unaosababisha kuwashwa kwa ngozi na kujikuna kupita kiasi, ugonjwa huo ulipewa jina la 'Kwangua vocha'," alisema.

Anna alisema LHRC na LEAT wamepitia ripoti mbili kuhusu uchafuzi wa Mto Mara zilizotolewa na taasisi mbili za serikali; Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Victoria na kamati ya kitaifa iliyoundwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira, Dk. Seleman Jafo, akidai wamebaini zinakinzana. Mkurugenzi huo alirejea ripoti ya Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Victoria kwamba vifo vya samaki vilitokana na kuwapo kiwango kikubwa cha mafuta (oili na grisi) ilhali ripoti ya kamati ya kitaifa inasema samaki hao walikufa kutokana na uchafuzi uliotokana na sababu za kiasili na za kibinadamu ikiwamo kiwango kikubwa cha kinyesi cha mifugo na uozo wa mimea ndani ya mto, hasa mimea vamizi.

**HOJA 12**

Katika mkutano huo na wanahabari, Mkurugenzi Mtendaji wa LEAT, Dk. Rugemeleza Nshala, akiwasilisha mapendekezo ya taasisi hizo mbili, alisema haki ya kuishi na kufanya kazi katika mazingira yaliyo safi na salama ni haki ya msingi na lazima iheshimiwe na wote ikiwamo watendaji wa serikali, taasisi au kampuni binafsi.

Dk. Nshala ambaye ni Rais mstaafu wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), alisema hoja yao ya pili ni kukataliwa na kutupiliwa mbali kwa ripoti ya kamati ya Prof. Samuel Manyele kutokana na kile alichokiita kujawa upotoshaji juu ya sababu za uchafuzi wa Mto Mara.

"Makamu wa Rais ambaye ndiye waziri halisi wa mazingira nchini, aunde tume huru ya uchunguzi wa uchafuzi ikijumusha wanamazingira wanaoaminika na weledi weledi mkubwa kisayansi ndani na nje ya nchi," alisema.

Dk. Nshala aliitaja pengekezo lao la nne ni kuwasilishwa mara moja ripoti ya usafishaji wa maji machafu itolewayo kila mwezi ya mgodi wa dhahabu North Mara ambao mabwawa yake ya kuhifadhi maji machafu yako jirani na Mto Mara, eneo lililochafuliwa.

Aliitaja hoja yao ya tano ni kupimwa kiwango cha uchafuzi eneo husika ili kubaini kemikali na sumu zilizomo na la sita ni kuhojiwa bila vitisho wananchi wa maeneo husika pamoja na waathirika kujua kiwango cha athari.

Mkurugenzi huyo alisema pendekezo lao la saba ni serikali ichukue jukumu la kusafisha eneo hilo lililochafuliwa na kudai fidia za gharama kutoka kwa uchafuzi kama inavyoelekezwa kwenye kanuni za mazingira.

Hoja nyingine ni kutolewa haraka fidia na haki kwa waathirika na ya tisa ni kuwajibishwa kwa watendaji wote wa serikali waliohusika na uchafuaji wa Mto Mara na wale walioshindwa kuchukua hatua dhidi ya uchafuzi uliotokea katika eneo hilo kuanzia mwaka 2018 hadi mwaka huu.

Pendekezo la 10 la taasisi hizo ni kuundwa upya kwa Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kutokana na kile ambacho Dk. Nshala alikiita kushindwa kuchukua hatua stahiki za kupambana na uchafuzi wa mazingira katika eneo la Mto Mara. "Kutengwe bajeti kubwa ya kutoa elimu na miundombinu ya kukabiliana na uchafuzi wa mazingira nchini," Dk. Nshala alisema.

Alilitaja pendekezo lao la 12 ni hatua madhubuti zichukuliwe na serikali kuwanusuru wakazi, mifugo na mazingira ya Mto Mara na Ziwa Victoria kwa ujumla kutokana na uwapo wa athari zinazoendelea kutokea maeneo hayo.

**ACT YATAKA UCHUNGUZI**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema kuna haja ufanyike uchunguzi upya kupitia taasisi huru ya uchunguzi na matokeo yake kuwekwa wazi mapema kuhusu uchafuzi wa maji kwenye Mto Mara. Pia kimesema kuna haja zichukuliwe jitihada za makusudi na haraka kudhibiti uchafuzi uliojitokeza kwa kusafisha maji kwa kutumia kemikali na dawa stahiki za kusafishia maji zinazotambulika na mamlaka ya usafishaji maji kwa matumizi halali ya binadamu, viumbe waishio majini pamoja na mimea na wanyama.

Msemaji wa Sekta ya Maji na Mazingira wa chama hicho, Ester Thomas, aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu suala hilo na kushauri kutolewa fidia kwa wananchi waliopata madhara yaliyotokana na uchafuzi huo wa maji na mazingira.

Vilevile, Ester alisema kuna haja watu walioathika na tukio hilo wapatiwe huduma za kiafya bila malipo, fidia kwa waliopoteza mifugo na ajira zao.

"Wapo walioathirika kwa kupoteza mifugo yao iliyokufa kutokana na kunyweshwa maji hayo, wavuvi walipoteza kipato kwa kuzuia shughuli za uvuvi kupisha uchunguzi. Wapo pia wananchi waliopata magonjwa ya mlipuko kutokana na athari za uchafuzi.

"ACT-Wazalendo tunaungana na wananchi wa Mara, wadau wote wa mazingira kuitaka serikali kulishughulikia suala hili linalogusa maisha ya watu, walioguswa na tatizo hili, hasa kwa wakazi wa Mara," alisema Ester.

Mwanzoni mwa mwezi huu kuliripotiwa uchafuzi kwenye Mto Mara uliosababisha samaki kufa na kuelea eneo la Kirumi Darajani wilayani Tarime.

# Samia aibua fursa ujenzi sekta binafsi

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan, ametangaza neema kwa sekta binafsi baada ya kutaka Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) na Watumishi Housing kushirikana na wawekezaji kuendeleza maeneo yote ambayo yako wazi.

Samia alitoa agizo hilo jana wakati akizindua nyumba 644 za makazi za Magomeni Kota, mkoani Dar es Salaam, zilizojengwa kwa gharama ya Sh. bilioni 52.195.

Akijibu ombi la TBA la kutaka kuwezeshwa ili kujenga maeneo mengine, Rais Samia alirudia kauli yake aliyowahi kuitoa awali kuwa popote ambapo sekta binafsi inaweza kuweka fedha, serikali itajitahidi kutoa nafasi kwao.

Rais alisema sekta binafsi iko tayari kushirikiana nao na kujenga maeneo yote ambayo watasema yanahitaji kujengwa.

"Jambo la maana ni kukaa na kukubaliana mikataba yenye tija baina yenu (TBA) na sekta binafsi. Niwaombe TBA na NHC, Watumishi Housing kaeni na sekta binafsi ya ndani au nje ya nchi mkubaliane kuyaendeleza maeneo yote ambayo yako wazi na yanapaswa kuendelezwa.

"Kwa sababu tukisema tuendeshe serikali itatuchukua muda mrefu kutafuta fedha serikalini za walipakodi tujikusanye, tuchange ziletwe mjenge, itatuchukua muda, lakini sekta binafsi iko tayari kutoa hizo fedha," alisema.

Rais Samia alisema benki ziko tayari kutoa hizo fedha kwa masharti ambayo watakubaliana nayo.

"Niyaombe mashirika ambayo tumeyapa dhamana ya kuendeleza makazi bora ama kwa wafanyakazi au wananchi mjumuike na sekta binafsi ili tupate maendeleo ya haraka," alisema.

Kuhusu nyumba za Magomeni Kota alizozizindua, Rais Samia ameridhia wananchi wauziwe kwa utaratibu wa mpangaji mnunuzi ili kurejesha gharama za ujenzi wake pekee bila kuwatoza gharama ya ardhi kwa sababu wakifanya hivyo watashindwa kuzinunua.

"Kwa wale wanaotaka kuweka fedha yao polepole waanze kulipa kuanzia sasa itakapofika miaka mitano umemaliza au kama unaendelea kulipa utaendelea wakati upo kwenye nyumba, mkianza wote kulipa sasa mtaifanya TBA ikusanye fedha za kumalizia eneo lililobaki. Anzeni kulipa sasa," alisema huku akiitaka TBA ihakikishe inamalizia eneo lililobaki kwenye nyumba hizo. "Ninawapongeza (TBA) kwa kupata wazo la kuweka Machinga Compex hapa na wazo la maduka makubwa na maegesho ya magari. Mjenge maegesho ya magari na kisasa yatakazoweka magari mengi ili tupunguze vurugu barabarani kwa wanaoegesha maeneo yasiyo rasmi," alisema.

Rais Samia alionyesha kuridhishwa na ujenzi wa nyumba hizo na kusema zimejengwa kisasa na zitakidhi mahitaji ya wananchi watakaokaa hapo.

Alitaka utunzaji wake kwa kuwa serikali imefanya yote ambayo wananchi waliomba ikiwamo kupewa kipindi cha kupumzika kuchangia huduma za uendeshaji wa nyumba ambacho kimetolewa kwa miezi mitatu.

"Kwa sababu watu wengi watakaa hapa, usafi unaweza kuwa tatizo hasa maeneo ya korido na ngazi naomba msimamizi wa nyumba uliyepewa usemaji wa nyumba hizi mtengeneze kamati za kusimamia usafi," aliagiza.

Rais Samia aliwaeleza wananchi watakaoingia kwenye nyumba hizo kuwa kutakuwa na michango kidogo ya kuendesha huduma za lifti na mitambo katika nyumba hizo. Pia alisema hatarajii wakazi wake kutumia kuni kupikia ndani ya majengo hayo au kutwanga kisamvu humo.

Mtendaji Mkuu wa TBA, Msanifu Majengo Daud Kondoro, alisema eneo hilo lina viwanja vitatu vyenye ukubwa wa hekta 12.9 (sawa na hekari 32) na zilizojengwa hadi sasa ni ekari tisa na lipo eneo la kwa ajili ya makazi, biashara na ofisi na la wazi kwa ajili ya maegesho ya magari, michezo na kupumzika.

# Lowassa apewa tuzo ya kimataifa

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu wa zamani, Edward Lowassa, ametunukiwa tuzo ya kimataifa kwenye maadhimisho ya Wiki ya Kimataifa ya Maji mjini Dakar, Senegal.

Tuzo hizo zilitolewa juzi na Baraza la Mawaziri la Maji la Afrika (AMCOW) kwa waasisi wake waliounda baraza hilo miaka 20 iliyopita.

Akizungumza kwenye hafla hiyo, mtoto wa Lowassa, Fred Lowassa, aliyeteuliwa kutoa shukrani kwa niaba ya wapokeaji tuzo wengine, alisema:

"Nipo hapa leo kupokea tuzo kwa niaba ya baba yangu. Ni bahati mbaya hayuko vizuri kwa sasa, amelazwa hospitalini lakini tunaamini kwa maombi yenu ataamka tena na kulitumikia taifa lake."

Alisema kipaumbele cha baba yake kilikuwa maji na elimu, jambo lililomsukuma katika uongozi wake akiwa Waziri wa Maji kwenda Misri kupigania matumizi ya maji ya Ziwa Victoria kwa wote ili kukomboa kinamama ambao kwa jitihada zake hizo, zaidi ya vijiji 500 Kanda ya Ziwa ni wanufaika wa maji hayo.

"Baba yangu angekuwa hapa leo (juzi) ninaamini angekuwa na mengi ya kuzungumza na wenzake juu ya safari yao ya miaka 20 ya AMCOW.

"Mimi nikiwa Mbunge wa Monduli kwa sasa, ambapo baba yangu alikuwa mbunge kwa zaidi ya miaka 20, aliapa kuwaletea maji wana Monduli, ADB (Benki ya Maendeleo Afrika) ilitoa msaada uliosaidia sana," Fred alisifu.

"Lakini kutokana na hali ya Monduli, bado kinababa na kinamama wanaendelea kutembea umbali mrefu kutafuta maji.

"Niseme hapa leo (juzi), Monduli inahitaji AMCOW, Tanzania inataka AMCOW na Afrika inataka AMCOW," Fred alihitimisha.




Watoto wa Waziri Mkuu mstaafu Edward Lowassa, Fred Lowassa (wa pili kulia) na Pamella Lowassa (kulia), wakiwa na tuzo aliyopewa baba yao, katika picha ya pamoja washindi na wawakilishi wa washindi kutoka mataifa mbalimbali ya Afrika, wakati wa hafla ya utoaji tuzo kwenye Wiki ya Maji Kimataifa, mjini Dakar, Senegal. Tuzo hizo, zimetolewa na Baraza la Mawaziri la Maji la Afrika (AMCOW) kwa waasisi wake, waliounda Baraza hilo miaka 20 iliyopita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri awatoa hofu Watanzania kuhusu kirusi kipya UVIKO - 19

**Na Mary Geofrey**

SERIKALI imesema kirusi kipya cha UVIKO-19 kilichothibitishwa na Shirika la Afya Duniani (WHO), bado hakijaingia nchini.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alithibitisha hilo kwa waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, wakati akipokea dozi milioni moja za chanjo aina mpya ya Sinovac, kati ya dozi milioni nne zilizotolewa na Uturuki.

Alisema wataalam wa afya nchini, wamefanya utafiti kuhusu kirusi hicho kipya kinachojumuisha virusi vya Delta na Omicron, ambacho kimejiunda na kuwa Omicron BA.1 na kubaini bado hakuna mgonjwa aliyethibitika kuugua.

"Asubuhi nilikuwa naongea na WHO kwamba sasa nini kifanyike baada ya kuja kirusi, wakasema bado wataalam na timu ya WHO wanaendelea kufanya utafiti je ni kikali na kina madhara kiasi gani. Lakini habari njema ni kuwa niliwataka wataalam wapitie sampuli zote lakini tumebaini hatujakipata hiki kirusi kipya," alisema Ummy.

Alisema wataalam wa afya walichukua sampuli 26 na kuzifanyia uchunguzi wa kina na kubaini ni kirusi kile kile cha Omicron kilichopo nchini tangu mwishoni mwa mwaka jana.

"Kwa hiyo huyu kirusi bado hajaingia nchini kwetu lakini tuendelee kuchukua tahadhari na hii itatusaidia kama watu wengi watakuwa wamechanja," alisisitiza Ummy.

Alisema tayari kirusi hicho kimeshathibitishwa katika nchi za India, Afrika Kusini na nchi za Ulaya.

Kwa mujibu wa Ummy, WHO inafanya utafiti wa kufahamu ukali wa kirusi hicho kipya cha UVIKO-19 na kwa upande wa wizara yake inaendelea kufanya utafiti kuwapo kwa kirusi hicho nchini.

Ummy alisema jitihada kubwa zinazofanywa na serikali ni kuhakikisha wananchi wanapata chanjo ya UVIKO-19 na hakuna njia nyingine ya kukikwepa kirusi hicho kutokana na muingiliano wa mataifa mbalimbali duniani.

Alisema serikali ya Marekani imetoa msaada wa Sh. bilioni 57 kwa ajili ya mapambano dhidi ya UVIKO-19, hivyo watatumia mashirika mbalimbali yasiyo ya kiserikali katika kuendesha kampeni za chanjo katika mikoa 16 ili kufikia asilimia 70 ya Watanzania.

Alisema watu wengi wakipata chanjo watasaidia kupunguza madhara ya ugonjwa huo pindi utakapothibitika kuwapo nchini.

**TAARIFA KWA UMMA**

**1 Aprili 2022**

*Kutakuwa na mabadiliko ya bei kwa baadhi ya vifurushi.*

Kifurushi cha Azam Plus cha 20,000/- ***kitakuwa 23,000/- kwa mwezi*** na kifurushi cha Azam Pure cha 13,000/- ***kitakuwa 15,000/- kwa mwezi.*** Kifurushi cha Azam Pure kwa wiki cha 4,000/- ***kitakuwa 5,000/-.***



116770602

Vifurushi vingine vitabaki vile vile bila mabadiliko, Azam Lite 8,000/- kwa mwezi na Azam Play 35,000/- kwa mwezi.

azamtv

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,

**TANGAZO**

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya tarehe **24.03.2022** mnatangaziwa hadi **05.04.2022** kampuni ya **Spedag Interfreight** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Holili** kuelekea **Moshi**, gari hilo lenye namba za usajili: **KDB189J / ZG5310 KCW051Z / ZG2320 KCW052Z / ZG3212 KBQ 628Z / ZE 0941**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| **Urefu** | - | **Mita 28.4** |
| **Upana** | - | **Mita 5.0** |
| **Kimo** | - | **Mita 5.6** |

3. Njia itakayotumika: **Holili hadi Moshi kupitia Soweto,** gari litasafiri muda wa mchana tu **( Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni)**

216769502

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

## TANZANIA ELECTRIC SUPPLY COMPANY LIMITED

# TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Wananchi wote mnatangaziwa kwamba, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) litaondosha kwa njia ya mnada wa hadhara Magari, Pikipiki, Betri zilizotumika, Mafuta Machafu, Samani chakavu za Ofisi, Vifaa vya Ofisi, Vyuma Chakavu, Vifaa vya Umeme/scraps, Matairi na vifaa mchanganyiko mbalimbali chakavu katika Mikoa ya Dar es Salaam (Temeke, Ilala, Kinondoni Kusini na Kinondoni Kaskazini), Pwani, Vituo vya kuzalisha Umeme (Ubungo I, Ubungo II, Tegeta, Kinyerezi I na Kinyerezi II) na Makao Makuu katika tarehe na vituo kama inavyoonekana hapa chini.

Mnada utafanywa kwa wananchi wote isipokuwa vyuma chakavu, vifaa vya kielektroniki, mafuta machafu, betri zilizotumika na matairi yaliyotumika vitauzwa kwenye makampuni yenye vibali vilivyotolewa na waziri mwenye dhamana ya mazingira kwa kuzingatia matakwa ya sheria ya mazingira ya mwaka 2004 na kanuni zake kama "Environmental Management (Control and Management of Electrical and Electronic Equipment Waste) Regulations, 2021" na "The Environmental Management (Hazardous Waste Control and Management) Regulations, 2021"

## ORODHA YA VITUO AMBAPO MNADA UTAFANYIKA

KITUO NA. 1A: TANESCO HQ – UBUNGO Tarehe 08/04/2022

- VIFAA CHAKAVU MCHANGANYIKO MBALIMBALI NA MAGARI YA HQ - UBUNGO

| S/N | REG. NUMBER | MAKE/MODEL | ENGINE NUMBER | CHASIS NUMBER | YEAR OF PURCHASE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | SU 34120 | TOYOTA LANDCRIUSER | 1HZ0320110 | JT711PTA507015196 | 1999 |
| 2 | SU 38826 | TOYOTA HILUX | 2KD5387698 | AHTFR22G506044775 | 2011 |

KITUO NA. 1B: - UBUNGO I GAS PLANT Tarehe 08/04/2022

- VIFAA CHAKAVU MCHANGANYIKO MBALIMBALI

KITUO NA. 1C: UBUNGO II GAS PLANT Tarehe 08/04/2022

- VIFAA CHAKAVU MCHANGANYIKO MBALIMBALI

KITUO NA. 2A: KINYEREZI I GAS PLANT Tarehe 09/04/2022

- VIFAA CHAKAVU MCHANGANYIKO MBALIMBALI

KITUO NA. 2B: KINYEREZI II GAS PLANT Tarehe 09/04/2022

- VIFAA CHAKAVU MCHANGANYIKO MBALIMBALI

KITUO NA. 3A: KURASINI CENTRAL STORE Tarehe 10/04/2022

- VIFAA CHAKAVU MCHANGANYIKO MBALIMBALI

KITUO NA. 3B: TEMEKE REGIONAL STORE Tarehe 10/04/2022

- VIFAA CHAKAVU MCHANGANYIKO MBALIMBALI NA MAGARI YA TEMEKE

| S/N | REG. NUMBER | MAKE/MODEL | ENGINE NUMBER | CHASIS NUMBER | YEAR OF PURCHASE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | SU 36657 | QINGQUI | 157FM10421001142 | LAELYZ4006B930041 | 2003 |
| 2 | SU 34283 | SUZUKI HONDA | | | 2008 |
| 3 | SU 35892 | QINGQUI | 15FM10221000870 | LAELYZ4013B930139 | 2003 |
| 4 | SU 30988 | TOYOTA L/C | 1HD0060686 | HDJ800001950 | 1993 |
| 5 | SU 32724 | TOYOTA L/C | IHZ0150571 | HZJ800023691 | 1996 |
| 6 | SU 35928 | ISUZU PICKUP | 4JH1954605 | 166417 | 1993 |
| 7 | SU 33659 | MITSUBISH CANTER | 4d32908246 | F9635ec00318 | 1998 |

KITUO NA. 4A: ILALA REGIONAL STORE Tarehe 11/04/2022

- VIFAA CHAKAVU MCHANGANYIKO MBALIMBALI NA MAGARI YA ILALA

| S/N | REG. NUMBER | MAKE/MODEL | ENGINE NUMBER | CHASIS NUMBER | YEAR OF PURCHASE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | SU 33457 | MITSUBISH | 4D56V5M21W32 | K34TJUNSR | 1988 |
| 2 | SU 35910 | ISUZU PICKUP | 4JH1954688 | 166415 | 2003 |
| 3 | SU 32752 | TOYOTA S/W | 3L4027562 | LJTH0012472 | 1995 |
| 4 | SU 35920 | ISUZU PICKUP | 4JH1954534 | 166591 | 2003 |
| 5 | SU 31752 | TOYOTA HILUX | HZ0110332 | NZJ500018223 | 1994 |
| 6 | SU 33461 | MITSUBISH | 4D56JB6313 | JMYJNK340WP00333 | 1997 |
| 7 | SU 33458 | MITSUBISH/PUP | 4D58JB5260 | JMYJNK340WP00225 7 | 1997 |
| 8 | SU 34325 | SUZUKI MARUTI | G1BBN11430 | MC71040258585 | 2001 |
| 9 | SU 34326 | SUZUKI MARUTI | G13BBN111587 | MG711N0206577 | 2001 |
| 10 | SU 34327 | SUZUKI MARUTI | G53BBN111277 | MG71040206671 | 2001 |
| 11 | SU 36658 | QINGQUI | 157FMI062100003 | LAELYZ4026B930011 | 2006 |
| 12 | SU 32923 | YAMAHA | 2HA0334224 | 2HA033424 | 1996 |
| 13 | SU 35887 | QINGQUI | 157FM1022100349 | LAELYZ4003B930133 | 2003 |
| 14 | SU 34281 | SUZUKI | 137815 | TF125137664 | 2008 |
| 15 | SU 35888 | QINGQUI | 157FMI0221000910 | LAELYZ4093B930146 | 2003 |
| 16 | SU 32637 | YAMAHA | 3HA033585 | 3HA033535 | 1996 |

KITUO NA.4B: KINONDONI KASKAZINI REGIONAL STORE (MIKOCHENI) Tarehe 11/04/2022

- VIFAA CHAKAVU MCHANGANYIKO MBALIMBALI NA MAGARI YA KINONDONI KASKAZINI

# TANGAZO

| S/N | REG. NUMBER | MAKE/MODEL | ENGINE NUMBER | CHASIS NUMBER | YEAR OF PURCHASE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | SU 35601 | MITSUBISH P/U | 4D56A28753 | MMBDNK7402D21242 | 2001 |
| 2 | SU 35890 | QINCQI | 157FM10221000968 | LAELYZ4003B930147 | 2002 |
| 3 | AIR COMPRESSOR | ET258R | | | |

KITUO NA. 5: KINONDONI KUSINI REGIONAL STORE (MAGOMENI) Tarehe 12/04/2022

- VIFAA CHAKAVU MCHANGANYIKO MBALIMBALI NA MAGARI YA KINONDONI KUSINI

| S/N | REG. NUMBER | MAKE/MODEL | ENGINE NUMBER | CHASIS NUMBER | YEAR OF PURCHASE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | SU 33492 | MITSUBISH D/C | 4D56JB4930 | JMYJNK340IN900314 7 | 1997 |
| 2 | SU 33491 | MITSUBISH D/C | 4D56JB4745 | JMYJNK340WP00314 4 | 1997 |
| 3 | SU 34302 | SUZUKI MARUTI | G13BBN111290 | MG711NO208666 | 2000 |
| 4 | SU 34308 | SUZUKI MARUTI | G13BBN111411 | MG71INO208689 | 2011 |
| 5 | SU 34321 | SUZUKI MARUTI | G13BBM111299 | MG71IHD208675 | 2001 |
| 6 | SU 29118 | BAJAJ | M246A026433 | F24CA024792 | 1989 |

KITUO NA. 6A: TEGETA GAS PLANT - Tarehe 13/04/2022

- VIFAA CHAKAVU MCHANGANYIKO MBALIMBALI

KITUO NA. 6B: BAHARI BEACH YARD – Tarehe 13/04/2022

- VIFAA CHAKAVU MCHANGANYIKO MBALIMBALI

KITUO NA. 7 – CHALINZE – 14/04/2022

- VIFAA CHAKAVU MCHANGANYIKO MBALIMBALI NA MAGARI YA KIBAHA-CHALINZE

| S/N | REG. NUMBER | MAKE/MODEL | ENGINE NUMBER | CHASIS NUMBER | YEAR OF PURCHASE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | SU 35418 | MITSUBISH P/U | 4D56JR3454 | JMYJNK340W901267 8 | 1998 |
| 2 | SU 33878 | TOYOTA PICKUP | 3L3791668 | LN1060112578 | 1995 |
| 3 | SU 35600 | MITSUBISH P/U | 4D56BA2665 | MMBOWKT7402D025 386 | 2001 |
| 4 | SU 30855 | NOSAN LORRY | ND5085511 | UG78042585 | 1992 |
| 5 | SU 33460 | MITSUBISH | 4D56JB6064 | JMYJNK340W900331 7 | 1997 |
| 6 | SU 33338 | MITSUBISH | 6014879659 | FHZ15HA00261 | 1997 |
| 7 | SU 34303 | SUZUKI MARUTI | G13BBW111345 | MG71IW0208594 | 2001 |
| 8 | SU 34304 | SUZUKI MARUTI | | | 2001 |
| 9 | SU36659 | QINGQUI | 157FM10621000011 | LAELYZ4036B930003 | 2005 |
| 10 | SU 36663 | QINGQUI | 157FM10421001345 | LAEYZ4016B930033 | 2005 |
| 11 | SU 36662 | QINGQUI | 157FM10621000018 | LAELYZ404B930009 | 2005 |
| 12 | SU 36664 | QINGQUI | 157FM10421001340 | LAELYZ4066B930027 | 2005 |
| 13 | SU 34336 | SUZUKI HONDA | | | 2001 |
| 14 | SU 33572 | QINGQUI | 35690920448969 | WDB6751472U27483 8 | 1997 |
| 15 | GENERA TOR | ELEMAX | | | |
| 7 | GENERA TOR | ELEMAX | | | |

KITUO NA. 8 – KIBAHA Tarehe 16/04/2022

- VIFAA CHAKAVU MCHANGANYIKO MBALIMBALI

**MASHARTI YA MNADA**

1. Chombo/Kifaa kitauzwa kama kilivyo na mahali kilipo;
2. Mnunuzi atalazimika kulipa papohapo amana (deposit) isiyopungua asilimia ishirini na tano (25%) ya thamani ya Chombo/Kifaa alichonunua, na kukamilisha malipo yote katika muda wa siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya mnada. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hili atakosa haki zote za ununuzi wa Chombo/kifaa husika na amana iliyolipwa haitarudishwa;
3. Mtu yeyote atakaye tamka bei ya juu kisha akashindwa kulipa asilimia ishirini na tano (25%) ya bei aliyotamka, atachukuliwa kuwa ni mwenye kutaka kuvuruga mnada na hivyo hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake kwa mujibu wa sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
4. Mnunuzi atatakiwa kuondoa/kuchukua chombo alichonunua katika muda wa siku saba (7) kuanzia siku ya kukamilisha malipo;
5. Vyuma Chakavu vitauzwa kwa Wanunuzi wenye viwanda vya kuchakata chuma tu. Wanunuzi wa vyuma chakavu watatakiwa kuleta leseni za kuchakata chuma na leseni hizo zitakaguliwa kabla ya zoezi la mnada kuanza. Vile vile nakala ya leseni hiyo itabaki kwa Muuzaji kwa ajili ya kumbukumbu;
6. Gharama za kubadilisha umiliki ni jukumu la mnunuzi na atatakiwa kukamilisha taratibu za kumilikishwa chombo/kifaa/chuma chakavu alichonunua kwa mujibu wa Sheria ndani ya siku ishirini na moja (21);
7. Ruhusa ya kuangalia vyombo itatolewa siku (5) kabla ya tarehe ya mnada husika;
8. Mnada utaanza saa nne (04:00) kamili asubuhi katika kila kituo kwa mtiririko ulioonešhwa; Kwa vituo vyenye vituo vidogo yani A, B, C, mnada utaanza kituo A kufuatia B na baadaye C.
9. Wananchi wote mnakaribishwa kushiriki katika mnada huu wa hadhara.

**IMETOLEWA NA**
**MKURUGENZI MTENDAJI**
**SHIRIKA LA UMEME TANZANIA (TANESCO)**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Maboresho mazingira ya uchaguzi muhimu

**RAIS** Samia Suluhu Hassan amefungua pazia kwa ajili ya kuweka mazingira mapya ya demokrasia nchini hasa kwenye suala la siasa na uchaguzi, kutokana na maelekezo aliyotoa kwa kikosi kazi.

Kikosi kazi hicho ni kile kilichokabidhi kwake mapendekezo ya wadau wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa kikishauri harakati za kupata katiba mpya zianze baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Baada ya kupokea mapendekezo hayo, Rais alitaka kikosi kazi hicho kufanyia kazi maboresho yote yaliyomo ndani ya mapendekezo kisha baadaye kuangalia haja ya kurekebisha katiba yetu.

Rais alisema hivyo na kufafanua kuwa pengine inawezekana kusiwe na haja ya kuandika mpya, bali kurekebisha baadhi ya maeneo na hata kama tunaandika mpya, lakini kazi kubwa imeshafanywa kwenye maboresho.

Kwa kauli hiyo ya Rais, tunaona amefungua pazia ili kuweka mazingira mapya ya demokrasia na mfumo wa siasa nchini ingawa baadhi ya wadau wameonyesha kutoridhika na mapendekezo ya katiba mpya ambayo ndiyo sheria mama kusubiri uchaguzi wa mwaka 2025.

Wanaamini kwamba katiba ndiyo inayowezesha kufanyika kwa uchaguzi vizuri ambao hauna kasoro nyingi na malalamiko, lakini pia ni muhimu kutambua kuwa suala la katiba mpya ni la mchakato wa muda mrefu na halihitaji njia ya mkato.

Mfano mzuri ni nchi jirani ya Kenya ambayo imewahi kufanya mchakato wa katiba mpya na kuipata ambapo ilichukua muda wa miaka mitano baada ya vikao vya kila wakati vya Bomas ndipo ikapatikana, hivyo tunadhani suala la subira ni la muhimu.

Baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010, Serikali ya Rais Jakaya Kikwete ilianzisha mchakato wa katiba mpya kutokana na mambo yaliyojitokeza katika uchaguzi huo, ambapo alisema kuwa ulikuwa wakati mwafaka wa kufanya hivyo, kutokana na katiba ya sasa kutokidhi matarajio ya kizazi kijacho.

Hata hivyo, mchakato huo uliishia njiani na bila kufikiwa makubaliano miongoni mwa wajumbe wa lililokuwa Bunge Maalum la Katiba mwaka 2014 kabla ya uchaguzi Mkuu wa 2015.

Jambo ambalo tunadhani linafaa kufanywa na wadau wa demokrasia ya siasa ya vyama vingi nchini ni kukazania kuwapo kwa mabadiliko ya sheria mbalimbali za uchaguzi ili kufanikisha uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2024 na Uchaguzi Mkuu wa 2025.

Mwaka 2024 kuna uchaguzi wa serikali za mitaa, hivyo tunadhani kwamba, sheria zingebadilishwa kabla ya uchaguzi huo ili kuwapo mgombea binafsi, kura za urais ziwe ni kupata 50+1 ili kumfanya mgombea aliyeshinda kuchaguliwa na wengi tofauti na sasa ambapo unatumika mfumo wa mshindi achukue chote hata kama ameshinda kwa kura moja.

Kwa utaratibu huo, tunaamini kuwa mshindi atakuwa amepatikana kwa ridhaa ya Watanzania wengi na hivyo kuondoa malalamiko.

Lakini mambo mengine tunayoshauri wadau hao ni kuomba katiba ya sasa, ifanyiwe marekebisho ili ushindi wa Rais upingwe mahakamani na kuwa na tume huru ya uchaguzi inayotoa maamuzi bila kuingiliwa.


Ushauri wetu unatokana na kuwapo malalamiko kuwa uchaguzi si huru na haki, hivyo tunaamini wakiomba kurekebishwa katiba ya sasa na kuwapo tume huru inayoaminika kwa wagombea, vyama, wadau wa siasa na wapigakura hakutakuwa na malalamiko.

Lingine ambalo tunadhani ni vyema wadau hao wakaomba lirekebishwe, ni suala la mgombea kupita bila kupigwa, lakini pia Jeshi la Polisi kutoingilia mikutano ya vyama vya siasa.

Hivyo, badala ya kutaka katiba mpya kabla ya uchaguzi mkuu wa 2025, ni vyema wakakazania marekebisho hayo ya katiba ya sasa kabla ya uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka 2024.

Rais ameonyesha wazi kuwa ana nia ya kuweka mazingira mapya ya demokrasia, hasa kwenye suala la siasa na uchaguzi, hivyo ingekuwa ni vyema wadau wakatumia nafasi hiyo kuomba marekebisho hayo, na serikali ikayaridhia.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Tufuatilie utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika maeneo yetu

Na Sabato Kasika

**SERIKALI** imeweka umuhimu wa kwanza katika masuala ya utawala bora katika ngazi zote za uongozi, kwa lengo la kurahisisha upatikanaji taarifa mbalimbali za maendeleo na hata zinazohusu hujuma kwa mali za umma.

Hapa wananchi wanahusika kikamilifu kuanzia utunzaji wa miradi ya maendeleo katika maeneo yao na hata kutoa taarifa kwa mamlaka husika wanapoona miradi inahujumiwa.

Wananchi wanatakiwa kufanya hivyo, ili miradi hiyo iweze kuwanufaisha wao na vizazi vyao, hivyo hawatakiwi kufanya hujuma ama kuona baadhi ya watu wakihujumu huku wao wakiwa kimya.

Hata hivyo, ni bahati mbaya, baadhi yao hawatambui jukumu hilo na wanadhani hawawajibiki kutunza na kulinda miradi hiyo katika maeneo yao na wako tayari kuona ikihujumiwa bila ya kutoa taarifa.

Katika mazingira ya aina hiyo, kuna uwezekano wa miradi mingi kuendelea kuharibika ama kuharibiwa, huku wakishuhudia bila kuchukua hatua kana kwamba si wajibu wao kufanya hivyo.

Kwa mfano, kunaweza kuanzishwa mradi katika maeneo yao ukakamilika, lakini baada ya muda mfupi ukaharibika au kuharibiwa wao wakiwa kimya, bila kuchukua hatua za kuwezesha wahusika kuchukuliwa hatua za kisheria. Mtindo huo umechangia kuwa neemesha wajanja wachache ambao wamekuwa wakitumia fedha za umma vibaya katika kusimamia miradi ya maendeleo hadi pale viongozi wa serikali kuu wanapobaini ubadhirifu.

Ninadhani kwamba, sasa umefika wakati kwa wananchi wenyewe kuchukua hatua tangu utekelezaji wa miradi unapoanza ili wajue utakavyokuwa hadi utakapokamilika, ili kujiridhisha miradi yenyewe itakuwa inalingana na kiasi cha fedha kilichotumika kuutekeleza.

Bila ya wananchi kuchukua hatua hizo na kusubiri viongozi wa serikali kuu au TAKUKURU kufanya uchunguzi, watendaji na watumishi wasio na uzalendo wataendelea kujineemesha kwa fedha za wavuja jasho.

Matukio ya matumizi mabaya ya fedha za umma yamekuwa yakiripotiwa katika maeneo mbalimbali, hivyo ni vyema jamii ikafuatilia miradi inayotekelezwa bila ya woga na kuchukua hatua pale inapokuwa na mashaka.

Ikumbukwe kuwa, kuna miradi mingi ya maendeleo hutekelezwa ikiwamo ya ujenzi wa zahanati, vituo vya afya, hospitali, shule, barabara na mingine mingi, hivyo ni vyema wananchi wasijiweke pembeni katika ufuatiliaji.

Kitendo cha wananchi kufuatilia miradi hiyo, kinaweza kusaidia kuokoa mamilioni ya fedha, lakini pia kufanya miradi itekelezwe kulingana na kiasi cha fedha kilichotolewa na siyo kuwa chini ya kiwango.

Ninaamini kwamba, iwapo watajiweka pembeni, watakuwa wanakwamisha maendeleo, lakini pia kujiweka katika mazingira hatari kutokana na miundombinu inayotekelezwa chini ya kiwango.

Kwa mfano, majengo ya zahanati, kituo cha afya au hospitali yakijengwa chini ya kiwango, yanaweza kuhatarisha usalama wa wananchi ikiwamo kuta kubomoka na kuwaangukia wanapokwenda kupata huduma za afya.

Ndivyo hivyo hata kwa madarasa, yanaweza kuangukia wanafunzi, au barabara zilizojengwa chini ya kiwango ili watendaji wapate kitu kidogo, zinaweza kusababisha ajali za magari na kupoteza maisha ya watu au kuwajeruhi.

Hivyo, ni muhimu wananchi kufuatilia kwa karibu miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa katika maeneo yao ili ilingane na kiasi cha fedha kilichotolewa badala ya kuchakachuliwa na wajanja wachache.

Wananchi kunyamazia au kutofuatilia miradi ya maendeleo kwenye maeneo yao, ni sawa na kuwaachia mwanya watendaji na watumishi wasio waaminifu kufanya hujuma katika miradi hiyo.

## Mamlaka za maji zatakiwa kupambana upotevu wa maji

Na Maulid Mmbaga

KATIBU Mkuu Wizara ya Maji, Anthony Sanga, amezitaka mamlaka za maji kuongeza nguvu zaidi katika kupambana na tatizo la upotevu wa maji na kufanya mapinduzi.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam wakati wa hafla ya mwendelezo wa uzinduzi wa taarifa ya utendaji kazi wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira, alisema suala la upotevu wa maji limezungumzwa sana, limepungua lakini sio katika viwango vya kuridhisha.

Aliwataka kuangalia njia zinazotoa mwelekeo mzuri ndani na nje ya nchi wajifunze na kuzitumia ili ziweze kuwasaidia kuondokana na changamoto hiyo, kwa kuwa jambo linalochangia upotevu wa maji ni mita.

"Sehemu mojawapo maji mengi yanapotea ni kwenye mita, nyingi zinaonekana haziko sahihi, inawezekana zinatuibia, zinatupunja kwasababu ingekuwa ni maji kumwagika basi kungekuwa na mabwawa mengi huko mjini.

Aliishauri bodi kufuatilia matumizi sahihi ya miongozo, ambayo bila kuifanyia kazi ni sawa na upotevu wa muda na rasilimali fedha.

Alisema, Rais Samia alitoa maelekezo ya kuwataka waendelee kutoa mita ambazo ni za malipo ya kabla ili waweze kupiga hatua zaidi katika sekta hiyo na kuwa tayari wameshaanza utekelezaji huo, katika mkoa wa Iringa wameshafungia wateja zaidi ya 5,000.

Aliipongeza Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) kwa kazi wanayoifanya ya kuchochea ufanisi wa mamlaka za maji na kuzifanya zipige hatua kiutendaji, huku akibainisha kuwa siku za nyuma kulikuwa na malalamiko mengi katika Wizara ya Maji na asilimia 64 ya malalamiko ya wateja yalikuwa ni kwenye bili.

"Kupitia mfumo ambao tumefunga una mabadiliko makubwa kwa kuwa mita inaposomwa mteja anatumiwa ujumbe wa maandishi aangalie unit kwamba ziko sana na ambazo msoma mita amezisoma, kama haupo sahihi maana yake atapiga simu afanyiwe marekebisho hivyo sitegemei mwisho wa mwezi bili inayotoka iwe ni bambikizi.

Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu EWURA, Mhandisi Exaud Fetaeli, alisema moja ya changamoto zinazoikabili mamlaka katika kuzitatua ni kiasi cha uzalishaji wa maji ambao haukidhi mahitaji, kwamba toka mwaka 2020-21 kiasi kilichofikiwa ni wastani wa asilimia 56.2 ya mahitaji ya maji katika miji ya makao makuu ya mikoa na miradi ya kitaifa.

## TCB yazindua kadi malipo kimataifa

Na Mwandishi Wetu

BENKI ya Biashara Tanzania (TCB) jana imezindua kadi ya malipo ya kidijitali ambayo itaisaidia serikali kufanikisha mpango mkakati wake wa kuifanya Tanzania kuwa na uchumi usiotegemea fedha taslimu.

Huduma hiyo inayojulikana kama Kadi ya Popote Visa ni matokea ya ushirikiano kati ya TCB na Visa International ya Marekani inayoongoza duniani katika teknolojia bunifu za malipo ya kidijitali.

Akizungumza wakati wa uzinduzi jijini Dar es Salaam, Ofisa Mtendaji Mkuu wa benki hiyo, Sabasaba Moshingi, alisema Popote Visa Card ina uwezo wa hali ya juu kusaidia kutimiza ndoto za taasisi hiyo ya kuendeleza huduma jumuisha za kifedha nchini.

TCB na mshirika wake wameazimia kuunga mkono juhudi za kitaifa za kujenga uchumi wenye matumizi madogo ya fedha taslimu kwa kuwekeza katika suluhisho bunifu za malipo ya kidijitali ambazo ni rahisi zaidi, salama na zinazozingatia ufanisi wa usimamizi wa fedha.

"Huduma kama kadi ya malipo ya kimataifa tuliyozindua leo na ushirikiano wetu na kampuni ya Visa ni muhimu katika juhudi za serikali kujenga uchumi wa kidijitali na kuifanya Tanzania kuwa taifa lisilotegemea sana malipo yanayofanywa kwa fedha taslimu," Moshingi alibainisha.

Aliwaambia waandishi wa habari kuwa uamuzi wa TCB kushirikiana na Visa unatokana na kampuni hiyo kuwa kigogo wa teknolojia za malipo duniani ikiwa na mtandao wa wafanyabiashara milioni 61 wa kimataifa.

Wakizungumza wakati wa uzindunzi huo, maofisa waandamizi wa Visa Afrika Mashariki, walisema dhamira ya kampuni hiyo si tu kuongeza matumizi ya kadi za kidijitali nchini peke yake bali duniani kote kuwahudumia wananchi, wafanyabiashara na serikali mbalimbali.

Makamu wa Rais wa Visa na Mkurugenzi Mtendaji wake wa Afrika Mashariki, Corine Mbiaketcha Nana, alisema Tanzania ina kila kitu kinachohitajika kuwa uchumi wa kisasa zaidi wa kidijitali.

"Kama suluhisho zote bunifu za malipo ya kidijitali, matumizi ya Popote Visa Card yana manufaa mengi na faida kubwa kwa watu binafsi, mashirika na serikali,"

Nana alifafanua na kusisitiza kuwa mchango wake mkubwa hasa kwa wananchi wa kawaida ni maendeleo ya huduma jumuishi ya kifedha.

Uzinduzi wa UCB Popote Visa Card umefanyika wiki mbili bada ya serikali kutangaza mipango na uwekezaji wake kwenye ujenzi wa uchumi usiotegemea sana fedha taslimu kupitia Mpango wa Tanzania ya Kidijitali.

Kwa mujibu wa Waziri wa Habari, Nape Mnauye, hivi karibuni Tanzania ilipata mkopo nafuu kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya utekelezaji wa azma hiyo wenye thamani ya dola za kimarekani milioni 150.

Wakizumgumza kwa nyakati tofauti wakati wa uzunduzi wa bidhaa hiyo mpya sokoni wateja na wandau mbalimbali wa TCB walisema kuzinduliwa kwa kadi hiyo mpya kutasaidai michakato mbalimbali ya kuharakisha maendfeleo ya kidijitali nchini.

"Ushirikiano wa kimkakati kati ya TCB na Visa sio tu unazinufaisha taasisi hizo mbili pekee, bali pia utasaidia kupanua wigo wa malipo ya kidijitali nchini na kuongeza faida za kibiashara katika nyororo wa thamani wa malipo kitaifa," Meneja Mkuu wa DT Card Tanzania, Christian Wielenga, alibainisha.

## Uturuki yaipa Tanzania dozi milioni 1 chanjo UVIKO

Na Mary Geofrey

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, amepokea ufadhili wa chanjo mpya aina ya Sinovac, dozi milioni moja kati ya milioni nne zilizotolewa na nchi ya Uturuki.

Chanjo hizo zinatarajiwa kupokelewa kwa awamu nne na zitachanja Watanzania milioni mbili. Akizungumza baada ya kupokea chanjo hizo jana katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere,

Ummy alisema ni kwa mara ya kwanza Tanzania inatumia aina hiyo ya chanjo tangu kuanza kutoa huduma hiyo nchini Julai, mwaka jana.

"Mapokezi ya chanjo hizi leo (jana) yanafanya jumla ya tulizopokea nchini tangu kutoa chanjo dhidi ya UVIKO-19 kuwa dozi milioni 10.8 aina ya Sinorpham, Janssen, Moderna, Pfizer na Sinovac ambazo zinatosha kuchanja watu 6, 381, 327," alisema Ummy.

Alifafanua kuwa, serikali itaendelea kutoa chanjo ya UVIKO-19, katika vituo mbalimbali vya kutolea huduma za afya nchini, kwa mujibu wa miongozo iliyoko zikiwamo huduma za mkoba na tembezi.

Kuhusu idadi ya Watanzania waliochanja, Ummy alisema hadi kufikia Machi 21 jumla ya watu 3,016,551 wamepata chanjo kamili kati ya watu 30,740,928 wenye umri wa miaka 18 na kuendelea.

"Nichukue fursa hii kuendelea kuwasisitiza viongozi na watendaji wa ngazi zote kutoa ushirikiano wa hali ya juu, ili kuhakikisha kuwa wananchi wanaendelea kuhimizwa kwenda kwenye vituo vya huduma za afya ili wakapate elimu kuhusu umuhimu wa chanjo na kisha kuchanja," alisema Ummy.

Aliwahimiza wananchi kuendelea kuchukua hatua mbalimbali za kujikinga dhidi ya UVIKO-19 ikiwamo uvaaji barakoa na kunawa mikono kwa maji na sabuni, kutumia vitakasa mikono na nyinginezo ambazo wataalamu wa afya wamekuwa wakiendelea kuzisitiza.

Alisema katika kufikia kuikinga jamii dhidi ya UVIKO-19 serikali inalenga kuchanja asilimia 70 ya Watanzania kuanzia miaka 18 hadi kufikia mwisho wa mwaka huu.

Ummy alisema watatoa huduma ya chanjo kwa kuwafuata wananchi katika vituo vya mabasi, daladala, nyumbani na maeneo ya mikusanyiko ili kufikia lengo hilo.

"Wakuu wa mikoa yote nchini ongezeni juhudi za uhamasishaji jamii ili kuongeza kiwango cha utoaji wa chanjo na kuhimiza wananchi wakapate chanjo kama inavyoshauriwa na wataalamu," alisema Ummy.

Aliwahamasisha watoa huduma za afya nchini, wachanje na waendelee kutoa elimu ya umuhimu wa chanjo kwa wananchi ikiwa ni pamoja na kuwashirikisha wahudumu wa afya ngazi ya jamii, wajumbe wa kamati za afya msingi na viongozi mashuhuri wakiwamo viongozi wa dini.

Kwa upande wake, Meneja Mpango wa Taifa wa Chanjo, Dk. Florian Tinuga, alitaja sababu za idadi ndogo ya Watanzania kujitokeza kuchanja licha ya juhudi zinazofanywa na serikali kuwa ni mitizamo na imani potofu zinazowasumbua wengi wao.

Alisema pia wananchi wanataka kufuatwa nyumbani na kwenye shughuli zao; wananchi kutokuwa na hofu ya ugonjwa na wengi kuamini kuwa chanjo inahitajika baada ya mtu kuugua.

Kwa upande wake, Balozi wa Uturuki nchini Tanzania, Mehmet Gulluogu, alisema ushirikiano mzuri wa mataifa hayo mawili, umewezesha kutoa idadi hiyo ya chanjo kwa ajili ya kudhibiti kuenea kwa maambukizi ya UVIKO-19.

Alisema nchini Uturuki asilimia 75 wamepata chanjo ya UVIKO-19 na juhudi zinaendelea za kuhakikisha wananchi wote wanapata huduma hiyo.


CAVEAT EMPTOR—BUYER BEWARE: *All that Landed Property Described as:*

CT No 113 985 Plot No 281 Block 'B' Tegeta Area' the property' of then Minors and Registered Joint owners , both of P o box 512 Tegeta Area,-Dar es salaam

Purported Planned Auction of '*Mortgaged* 'Property SUBJECT OF ONGOING LITIGATION

CT No 113 985 Plot No 281 Block 'B' Tegeta Area' the property' in the Name of then Minors].

Notice is hereby given and the General pubic is cautioned as follows:

1.0. That the above property has since 2017 been subject of court litigation in Land Application No 384 of 2017 in the District Lands& Housing Tribunal-Kinondoni-Dar es salaam against

Commercial Bank of Africa Tanzania Limited------------------*[1st Respondent]*

Now NCBA Bank Tanzania Limited, and

Elizabeth Elinami Mkony------------------------------------*[2nd Respondent]*.

2.0. That there are actual joint registered owners of the property, then minors, who in court claim Fraud and Contest never mortgaging the same in bank's favor nor it being compliant;

3.0. That since then there is pending a court dispute regarding the LEGALITY of the said mortgage;

4.0. That the said property has been subject of serial court orders and litigation restraining disposition till final disposal of the said main dispute which was recently by both parties' consent fixed for hearing;

5.0.That notwithstanding the above, it has come to the attention of joint registered owners and has emerged public notice(s) that the suit property will be disposed by way of auction on 29/3/22;

6.0. That results thereof the general public and would be bidders or buyers are further Notified and strongly Cautioned as follows:

6.1.That subject to pending determination of the registered owners' and the bank's, if any' proprietary rights and interests, it is seriously CONTEMPTOUS of the Court and CRIMINAL to purportedly instruct and conduct property auction or disposition, that may also result in breach of peace and personal liabilities of principal officers and other individuals, AND;

6.2.It is contemptuous, too, to be privy or party to its disposition as No lawful title will pass to any person or any third party nor would defence of *bonafide purchaser for value* apply leading even into risky and protracted further litigations from all other parties.

REMAIN CAUTIONED & ADVISED

By Joint Registered Owners of the Property Dated at Dar es salaam This:23/03/2022

# EU yaitaka Urusi kusitisha mapigano Ukraine

**Na Beatrice Shayo**

UMOJA wa Ulaya (EU) umeitaka nchi ya Urusi kusitisha mapigano nchini Ukraine kuepusha madhara kwa dunia.

Hayo yalisemwa juzi jioni jijini Dar es Salaam na Balozi wa Ufaransa, Nabil Hajlaoui na balozi wa EU nchini, Manfredo Fanti, wakati wakizungumza na waandishi wa habari kuhusiana na yanayoendelea kati ya Ukraine na Urusi.

Mkutano huo ulihudhuriwa na mabalozi mbalimbali wanaoziwakilisha nchi zao nchini, wanachama wa Umoja wa Ulaya.

Balozi Fanti alisema kuendelea kwa vita hivyo kumeshaanza kusababisha madhara duniani ikiwamo kupanda kwa bei ya nishati, mafuta na usambazaji wa bidhaa kutoka nchi moja kwenda nyingine.

Alisema nchi za Ulaya zinaitaka Urusi kusitisha mapigano kwa sababu hukumu iliyotolewa na Mahakama ya Kimataifa Machi 2 na 16, mwaka huu iliitaka Urusi kusitisha vita na kuondoa vikosi vyake nchini Ukraine.

Alisema nchi za Ulaya zimechukua hatua mbalimbali kuonyesha kutoridhishwa na vita hiyo ikiwa ni pamoja na kuwawekea vikwazo mbalimbali vya kiuchumi na biashara.

Balozi wa Ufaransa, Nabil Hajlaoui, alisema lengo la Umoja wa Ulaya ni kuona haki inapatikana kwa njia ya mazungumzo na kuziomba nchi za Afrika ikiwamo Tanzania kuungana mkono Umoja huo kuhimiza kupinga vita hiyo.

Alisema Ufaransa na Umoja wa Ulaya wanalaani vikali mashambulizi ya kijeshi ya Urusi nchini Ukraine ambalo ni shambulio kubwa zaidi walilolifanya.

Kadhalika, alisema nchi za Ulaya hazitaki vita wala kuivamia Urusi, zinataka itumike njia bora ya kusitisha mapigano hayo ambayo mpaka sasa yamesababisha mamilioni ya wananchi wa Ukraine kukimbia nchi yao na kuwa wakimbizi katika nchi za Ulaya.

Balozi wa Poland nchini, Krzysztof Buzalski, alisema mpaka sasa hivi nchi yake imepokea zaidi ya wakimbizi milioni mbili kutoka Ukraine na makadirio yaliyofanywa na Umoja wa Ulaya wiki hii yanaonyesha kama vita haitasitishwa watapokea wakimbizi milioni nane kutoka nchini humo.

Alisema maofisa uhamiaji wa Poland wanaenda kwenye mpaka wa Ukraine na Urusi na wanajitahidi kutoa huduma nzuri kwa wanaokimbia vita ikiwamo watoto, wanawake, wagonjwa, wazee na wanafunzi ili kuhakikisha wanavuka salama.

Balozi alisema wanafunzi wanaotoka nchi za Afrika ikiwamo waliotoka Tanzania walisaidiwa kuvuka salama na wamepatiwa hifadhi nchini Poland.




Balozi wa Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU) nchini Tanzania, Manfredo Fanti (kushoto), akizungumza katika mkutano na mabalozi wa Ulaya hapa nchini, jijini Dar es Salaam juzi, kupinga vita vinavyoendelea nchini Ukraine, vinavyofanywa na nchi ya Urusi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# DC awabana makandarasi maji

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

SERIKALI wilayani Kahama mkoani Shinyanga imetangaza kuwanyima miradi makandarasi wanaoshindwa kumaliza kazi kwa wakati na kusababisha wananchi kuendelea kutumia maji ya visima.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga, alisema hayo juzi wakati wa ziara ya kukagua miradi ya maji katika Halmashauri za Msalala na Ushetu.

Katika ziara hiyo Kiswaga alibaini baadhi ya miradi hiyo imeshindwa kukamilika kwa uzembe wa makandarasi waliopewa kazi na serikali.

Alisema kuna baadhi ya miradi ya maji katika Halmashauri ya Msalala ilianza mwaka 2018, lakini mpaka sasa haijakamilika kutokana na makandarasi kushindwa kuwasilisha hati za malipo ili walipwe.

Kiswaga alisema atawachukulia hatua za kisheria makandarasi wanaotekeleza miradi hiyo nje ya muda kwa kuwazuia kuendelea kupata kazi zingine.

"Nahitaji miradi yote ya maji inayoendelea kujengwa wilayani kwangu ikamilike ifikapo Aprili 30, mwaka huu. Nje ya hapo nitawajibisha makandarasi kwa kuwanyang'anya tenda na kuwapiga marufuku kupata tenda nyingine labda mpaka nitakapoondoka wilaya hii," alisema Kiswaga.

Kaimu Meneja wa Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Paschal Mnyeti, alisema moja ya sababu zinazofanya makandarasi kushindwa kukamilisha miradi hiyo kwa wakati ni ucheleweshaji wa malipo kwa kila hatua ya ujenzi wanayofanya.

Alisema wao kama watendaji, wamekuwa wakipokea hati za malipo na kuziwasilisha makao makuu kwa ajili ya malipo, lakini zinachelewa kulipwa na kwamba wataendelea kufuatilia kutatua tatizo hilo ili ujenzi usisimame.

Akizungumza kwa niaba ya makandarasi wanaotekeleza miradi ya maji Ushetu, John Panga alisema maagizo ya mkuu wa wilaya wameyapokea na watahakikisha wanakamilisha miradi yote ya maji.

# Mwili wa kichanga waokotwa jalalani

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

MWILI wa mtoto mchanga anayekadiriwa kuwa na miezi saba, umeokotwa jalalani katika mtaa wa Mama Farida Kata ya Nyasubi, Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga.

Mtoto huyo aliokotwa kwenye jalala hilo jana majira ya asubuhi na kuzua taharuki kwa wakazi wanaoishi maeneo hayo bila kujua ni nani aliyefanya kitendo hicho.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Nyasubi, Leonard Mayala, alisema tukio hilo la kutupa vichanga kwenye eneo hilo ni la pili na kuwataka wananchi kushirikiana na Jeshi la Polisi kubaini aliyefanya vitendo hivyo vya ukatili.

Mayala alisema matukio hayo ambayo yamekuwa yakitokea katika eneo hilo la jalala kubwa la takataka lililoko katikati ya mji wa Kahama, yamekuwa yakiwashangaza wananchi na kuomba uongozi wa Manispaa ya Kahama kulihamisha.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Manispaa ya Kahama, Dk. George Masasi, alikiri kupokea mwili wa kichanga hicho kikiwa kimekufa na kusema taratibu zingine za kiuchunguzi zinaendelea kwa kushirikiana na polisi.

Baadhi ya wananchi na wakazi wa eneo hilo walisema tukio hilo ni mwendelezo wa matukio ya namna hiyo yanayosababishwa na malezi mabaya ya wazazi ikiwa ni pamoja na mimba zisizotarajiwa.

Walisema kuwa tabia ya wanaume kuwarubuni watoto wa kike na kuwapa ujauzito na kisha kuwatelekeza inachangia kuwapo vitendo hivyo.

Waliongeza kuwa tukio hilo ni la pili katika eneo hilo katika kipindi kifupi kilichopita na kuomba uchunguzi ufanyike ili kuwabaini wahusika.

"Sisi wananchi ambao tumekuwa tukiishi katika eneo hili tumekuwa tukilalamika kila siku kuhusu kuondolewa kwa jalala hili ambalo limekuwa ni kero kwetu kwani matukio mengi ya ajabu yamekuwa yakifanyika eneo hili ikiwa ni pamoja kutupwa watoto," alisema mmoja wa wananchi hao.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, George Kyando, alisema tukio hilo bado halijafika mezani kwake na kuongeza kuwa kwa sasa matukio kama hayo yanazidi kuongezeka.

# Bodi ya TRA yavutiwa na uwekezaji wa SBL

**Na Mwandishi Wetu**

BODI ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) imeelezea kuridhishwa na uwekezaji

unaofanywa na Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL) kwenye upanuzi wa biashara zake na katika miradi ya kusaidia jamii.

Akiongeza wakati bodi hiyo ilipotembelea kiwanda cha kampuni hiyo Dar es Salaam kuangalia utekelezaji wa mfumo wa stempu za kielektroniki unavyoendelea, mwenyekiti wa bodi hiyo Ulledi Mussa alisema uwekezaji unafanywa na SBL unatija kubwa kwa taifa.

"Upanuzi mkubwa wa viwanda vyenu unaonyesha kuwa mpo na mtaendelea kuwapo. Serikali ipo nyuma yenu na changamoto mbalimbali za kikodi zitakuwa zikiendelea kufanyiwa kazi ili

kuwawekea mazingira mazuri zaidi ya kufanya kazi," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema kuwa TRA inaichukulia kampuni ya SBL kama mdau muhimu wa maendeleo na kushukuru kwa uwekezaji wake katika miradi mbalimbali ya kijamii.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Mahusiano kwa Umma wa SBL, John Wanyancha, alisema kampuni

hiyo mwaka jana ilizindua mradi mkubwa wa uwezaji ambao utakaogharimu shilingi bilioni 166, na kuongeza kuwa uwekezaji huo unahusisha upanuzi wa viwanda vyake pamoja na ujenzi wa kiwanda cha kuzalisha pombe kali.

Alisema mradi huo ulioanza mwaka 2019 utaiwezesha kampuni hiyo kuongeza uzalishaji wa bia katika viwanda vyake vya Dar es Salaam, Mwanza na Moshi na kuongeza kuwa SBL imajenga kiwanda cha kuzalisha pombe kali kilichoko Moshi ikiwa ni sehemu ya uwekezaji huo na kufafanua kuwa kiwanda hicho kinaendeshwa na wanawake watupu.

"Upanuzi tunaoufanya utapelekea kuongezeka kwa mahitaji ya nafaka ambazo SBL hununua kutoka kwa wakulima wazawa kama shayiri, mahindi na mtama kwa ajili ya kuzalisha bia zetu. Upanuzi pia

utatengeneza ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja na kuongeza usambazaji wa bidhaa zetu sehemu mbalimbali hapa nchini. Hii itasaidia kuongeza kodi tunazolipa serikalini," alisema na kuongeza:

"Pamoja uwekezaji huo mkubwa wa upanuzi, Wanyancha alisema SBL pia imekuwa ikifadhili miradi

mbalimbali ya kusaidia jamii ikwamo miradi ya maji ambapo zaidi ya watu milioni mbili wamenufaika na miradi hiyo.

"Pia tuna programu nyingine kama kilimo viwanda ambapo tunatoa ufadhili kwa wanafunzi wa kilimo kwa ajili ya kuongeza wataalamu."

## Radi yaua mama na mtoto Kigoma

**Na Deogratius Nsokolo,** KIGOMA

WAKAZI wawili wa kijiji cha Matyazo Kata ya Kalinzi wilayani kigoma, Berthania Zabron (44) na mwanawe Loveness Kulwa mwenye umri wa mwaka mmoja na miezi minane wamekufa kwa kupigwa na radi wakiwa shambani.

Katika tukio hilo, baba wa familia hiyo, Christophe Kulwa Abel alijeruhiwa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kigoma, Kamishna Msaidizi wa Polisi, James Manyama, alisema tukio hilo lilitokea juzi kufuatia mvua zinazoendelea kunyesha maeneo mbalimbali ya mkoa wa Kigoma.

Alisema mama huyo ambaye ni mtumishi katika Kituo cha Afya Matyazo na mwanawe walikufa papohapo huku majeruhi akipelekwa katika kituo hicho kupata huduma za afya, na kwamba anaendelea vizuri.

Aliwatahadharisha wananchi kuchukua tahadhari ya matukio mbalimbali kutokana na matukio ya ya radi katika mkoa huo.

Baba huyo wa familia alisema tukio hilo lilitokea majira ya mchana, baada ya kula chakula wakiwa shambani.

"Mke wangu alipika chakula akaniita wakati huo nilikuwa naendelea kulima, nikaenda tukakaa tukala na baada ya kula tukaendelea kukaa huku tukizungumza masuala mbalimbali, lakini ghafla radi ilipiga nami nikapiga kelele za kulalamika, watu wakaja na waligundua kuwa mke wangu na mtoto wamekufa," alisema Kulwa.

Katika tukio jingine, Kamanda Manyama alisema watu wawili Zuber Seleman na Ulimwengo Kametelo wamejeruhiwa, baada ya kupigwa na radi wakati wamejificha mvua kwenye nyumba ya Ulimwengu Kametelo kijijini hapo.

Alisema majeruhi hao wanaendelea vizuri na matibabu katika Hospitali ya Wilaya ya Kakonko.




Balozi wa Kampeni ya NMB MastaBata Kivyako Vyako, Masoud Kipanya (wa pili kulia), akipiga simu kwa mmoja kati ya wateja waliobahatika kushinda na kujinyakulia kitita cha sh. milioni tatu, wakati wa kuchezesha droo ya mwisho ya msimu wa tatu katika Tawi la NMB Sinza Mori, Dar es Salaam jana. Katika Droo hiyo jumla ya wateja 30 walizawadiwa fedha taslimu Sh. milioni tatu kila mmoja. Kushoto ni Mkuu wa Idara ya Wateja Binafsi Benki hiyo, Aikansia Muro, (wa pili kushoto) Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara, Filbert Mponzi na Meneja Mwandamizi kitengo cha Kadi, Manfredy Kayala. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# W/biashara Temeke watakiwa kutumia fursa mikopo midogo

**Na Mwandishi Wetu**

WANACHAMA wa Klabu ya Wafanyabiashara Wanaohudumiwa na Benki ya NMB, Wilaya ya Temeke, wametakiwa kutumia fursa zitokanazo na ongezeko la kiwango cha mikopo midogo ya kuanzia Sh. 500,000

hadi Sh. milioni 75 na kushuka kwa riba zake kutoka asilimia 21 hadi asilimia 14,

kujiimarisha kiuchumi.

Wito huo umetolewa na Meneja wa NMB Kanda ya Dar es Salaam, Donatus

Richard, wakati wa kongamano lililoshirikisha wanachama zaidi ya 150 wa klabu hiyo wilayani Temeke,

ambalo lilifunguliwa na Mwenyekiti wa klabu hiyo, Ezekiel Gutti.

Donatus alibainisha kuwa benki hiyo ambayo ni miongoni mwa benki zaidi ya 50 nchini, ina mtaji wa kutosha unaowapa wateja wao uhakika wa usalama wa fedha zao na usiri wa

taarifa zao. Na hii ndio imechangia zaidi ongezeko kubwa la kiwango cha mikopo

midogo, sambamba na kushuka kwa riba za mikopo hiyo.

"Endeleeni kutumia fursa hiyo muhimu ya mikopo, ambayo kwa wale wateja wanaochipukia, riba

imeshuka kutoka asilimia 21 ya awali na sasa kuwa asilimia 14. Huduma hizi zipo

matawini," alisema.

Donatus aliwataka wanachama hao kuwa mabalozi wema wa NMB katika jamii inayowazunguka, ili kuongeza idadi ya wanufaika wa huduma mbalimbali, kama za bima, zikiwamo za vikundi vya kuanzia watu watano na kuendelea, ambazo zinatoa kinga na kutoa fidia kwa mwanachama na familia (mke/mume na watoto) anapofariki.

# Bei bidhaa za nafaka zaendelea kupaa

**Na Suzana Makorongo**

BIDHAA za nafaka zimeendelea kupanda bei katika baadhi ya masoko mbalimbali jijini Dar es Salaam na kusababisha maisha kuwa magumu kwa wafanyabiashara na wanunuzi.

Baadhi ya masoko yaliyotembelewa na mwandishi wa habari hizi, likiwamo la Kisutu na Temeke, bei ya bidhaa hiyo imepanda zaidi ya Sh. 500 hadi 2,000 kutofautiana na bidhaa.

Lita moja ya mafuta ya kula ambayo ilikuwa ikiuzwa kwa Sh. 3,500- 4000 sasa hivi imepanda na kufikia Sh. 6,500-7000. Bei hiyo inategemea na kampuni inayozalisha bidhaa hiyo.

Aidha, unga wa sembe kilo moja iliyokuwa ikinunuliwa kwa Sh. 800-900 sasa inanunuliwa kwa Sh. 1,300 hadi 1,500.

Kwa upande wa mchele kilo moja iliyokuwa inanunuliwa kwa Sh. 1500-2000, sasa inanunuliwa kuanzia Sh. 2000 -2500, kutegemea na sehemu unakotoka.

Mwenyekiti wa wauza nafaka katika Soko la Kisutu, Mohamed Salum, aliiambia Nipashe kuwa baadhi ya wateja wanashindwa kununua kutokana na kukuta bei mpya kila wanapofika sokoni kupata bidhaa.

"Kwenye biashara kuna ushuru kama nilikua na wateja 10 najikuta nina wateja watatu mpaka wanne wanakimbia hali ya vitu iko juu sana."

Aliiomba serikali itoe bei elekezi kwa sababu wanaoteseka ni wauzaji na wateja.

"Tunapoteza wateja, Soko la Kisutu limekosa wateja kwa mwaka huu tofauti na miaka ya nyuma na sisi wafanyabiashara wa Kisutu mitaji yetu inakata tunapata hasara kila siku, wateja wamesusa kuja kwa ajili ya bei za nafaka kupanda bei," alisema Salum.

Mamalishe wanaofanya biashara ya chakula akiwamo, Halima Selemani, alisema biashara imekua ngumu tofauti na mwaka jana kutokana na vitu kupanda bei.

"Kwa sisi mamalishe biashara inakua ngumu siku hadi siku, wateja wanakimbia, mwaka jana sahani ya chakula tuliuza kuanzia Sh. 1,000-1500 kwa sasa sahani inabidi uuze Sh. 2000-2500 kwa sababu mchele wenyewe uko juu, unga na mchele bei moja."

Kwa upande wao wateja wanaokula kwa mama lishe, Amina Juma, alilalamika kupanda ghafla kwa bei ya chakula. "Kwa kitendo cha bidhaa kupanda bei kimesababisha sisi wateja wa ugali na wali kuuziwa sahani Sh. 2000-2500 wakati zamani ulikuwa Sh. 1,000 unakula na kushiba unaendelea na biashara zako sasa hivi unaona ushinde njaa ukale nyumbani na kufanya biashara na njaa ni ngumu sana," alilalamika.

Mnunuzi wa nafaka sokoni hapo, Lameck Isaya, aliomba serikali kuingilia kati kwa sababu haieleweki shida iko wapi mpaka vitu kupanda bei.

Alisema sasa hivi hata ukimuachia mke pesa nyumbani anakwambia nenda mwenyewe sokoni maana pesa haitoshi kuanzia mafuta mpaka unga vimependa bei.

Makamu Mwenyekiti wa Soko la Temeke Stereo, Kondo Miaka, aliiambia Nipashe kuwa bidhaa za nafaka kama mchele na maharagwe vimependa zaidi.

"Wakulima wanaoleta bidhaa hizo wanalalamika hawapati faida kutokana gharama za usafirishaji kuwa kubwa," alisema.

## 'Madereva bodaboda wapatiwe elimu usalama'

**Na Suzana Makorongo**

KUTOKANA na tamko lilitolewa na Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, kuhusu vijana wanaoendesha bodaboda kusababisha ajali nyingi barabarani, ombi limetolewa la kutoa elimu ya mara kwa mara kwa madereva hao kuhusu Sheria ya Usalama Barabarani.

Nipashe iliongea na baadhi ya madereva hao akiwamo John Lucas, ambaye anafanya shughuli yake kwenye fukwe ya Coco, Oysterbay jijini Dar es Salaam, na kukiri kuwa baadhi yao wanafanya kazi hiyo bila kupitia shule ya udereva na badala yake wanajifunza mtaani kwa wiki moja na kuanza kuchukua abiria.

"Ni kweli Waziri wa Afya aliyosema ni sahihi siye madereva wengi ndiyo chanzo cha ajali zinazotokea barabarani maana wengi wao hawajapitia chuo cha udereva, kajifunza wiki mtaani wiki ijayo yuko barabarani anapakia abiria ikiwa hata sheria ya udereva haifahamu kuna sehemu unaona kuna taa za kusimama yeye kwa kuwa hajasoma hajui nini maana ya taa anavuka anakumbana na lori anagongwa, tena kwa Dar es Salaam ni nyingi sana," alisema.

Aliiomba serikali kuendelea kutoa elimu ya udereva kwa madereva bodaboda ili kunusuru ajali nyingi kutokea ambazo zinasababishwa na wale wasiofuatia sheria za barabarani.

"Naiomba serikali au Waziri Ummy kwa kuguswa na hilo jambo wizara inayosimamia mambo ya usalama barabarani itoe mafunzo ya mara kwa mara na sheria kali iongezwe kwa madereva labda itasaidia kupunguza ajali," alisema Lucas.

Lucas alisema, kazi ya bodaboda imesaidia kutoa ajira kwa vijana, lakini wanaoitumia vibaya wanasababisha sekta hiyo kutothaminiwa na kuonekana madereva wote ni wahuni.

Abiria anayetumia usafiri wa bodaboda, Esta Msafiri, alisema kuwa bodaboda zinarahisisha safari, lakini ndiyo usafiri hatari zaidi.

"Kweli boda ni usafiri wa haraka tatizo ni kwamba madereva wake wengi hawako makini wanapokuwa barabarani na wengine hawajasomea udereva na sijui kwanini wanakuwa sio waangalifu na ukizingatia ndiyo kazi inayowaingizia kipato na kuweza kusaidia familia zao," alisema.

Alisema vijana wengine imewasaidia kuwaepusha na makundi ya uovu na tabia mbaya," alisema Msafiri.




Diwani wa Kata ya Kivukoni, Sharik Shoughule (wa pili kushoto), akikata utepe kuzindua boti mpya ya uvuvi yenye thamani ya sh. milioni 108, iliyotolewa na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, kama mkopo kusaidia kikundi cha Mzizima Fisheries katika Soko la Samaki Feri, jijini humo juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wanafunzi UDSM, UDOM wang'ara kwenye TEHAMA

**Na Mwandishi Wetu**

WANAFUNZI wa Kitanzania wa TEHAMA kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Dodoma waliibuka miongoni mwa wanafunzi bora zaidi katika shindano la TEHAMA Huawei 2021-2022 Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Likiwa na kaulimbiu ya "Connection, Glory, Future", shindano hilo lilihitimishwa Februari 19, huku zaidi ya nchi 15 na timu 38 zikifanya mitihani ya maandishi na maabara. Shindano hili lilivutia zaidi ya washiriki 15,000 kutoka Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Shindano la TEHAMA Huawei 2021-2022 Kusini mwa Jangwa la Sahara lilizinduliwa katika kanda ya Afrika miaka sita tu iliyopita, limekuwa shindano kubwa zaidi la ujuzi wa TEHAMA barani Afrika na duniani kwa ujumla.

Tanzania iliwakilishwa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Dodoma na kila timu ilikuwa na wanafunzi. Timu za Tanzania zilijishindia zawadi ya kwanza (Cloud Track), zawadi ya pili, na zawadi ya Tatu (Network Track). Wanafunzi hao ni Mafiu Khatibu, Daniel Mathew na Ndabuye Sengayo (UDOM), James Mushi, Erick Shemdoe, na Zuwena Hamoud (UDSM) na Joan Makyao, Kivuyo Kelvin, na Peter Edward (UDSM). Timu zote tatu zimeingia fainali za dunia zitakazofanyika nchini China mwezi Mei ikitanguliwa na hafla ya kukabidhi tuzo itakayofanyika nchini Afrika Kusini Aprili mwaka huu.

Akizungumzia mafanikio hayo Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi Zanzibar, Ali Khamis Ali alisema: "Kama nchi tunajivunia vijana hawa wenye vipaji kwa ushindi mkubwa walioupata katika Fainali za Kanda za Shindano la TEHAMA la Huawei, ushindi wao unathibitisha ubora wa kitaaluma wa vyuo vyetu vya elimu ya juu, tunatumai na kuamini watang'ara na kuwa mabalozi wazuri wa Tanzania, katika duru ya kimataifa.

"Naipongeza Huawei kwa mipango hii na tunatarajia kuona juhudi hizi zaidi na zaidi kwa mfumo wa ikolojia wa vipaji wa TEHAMA ulio imara na endelevu nchini."

Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa Huawei Tanzania, Tom Tao, aliwapongeza wanafunzi hao kwa ushindi wao mkubwa akisema; "Huawei Technologies itaendelea kushirikiana na serikali na Taasisi za Kitaaluma katika kutoa mafunzo ya TEHAMA kwa wanafunzi wa Kitanzania vijana na kuhakikisha kuwa maarifa na ujuzi wanaopata vijana hao ni muhimu katika kuchochea ukuaji wa Tanzania kijamii na kiuchumi".

Zuwena Hamoud Salum, mmoja wa wanafunzi wawili wa kike wa kwanza kushinda shindano la TEHAMA la Huawei aliwahimiza wanafunzi wa kike kushiriki katika shindano hilo huku akitoa shukrani zake kwa nafasi ambayo Huawei wamewapatia.

"Nawaomba na kuwahimiza wanafunzi wenzangu wa kike kuchangamkia fursa hizi zinazotolewa na Huawei kupitia shindano la TEHAMA la Huawei. Jukwaa hilo litawawezesha kuonyesha utaalamu wao wa TEHAMA na kuudhihirishia ulimwengu kuwa wanawake wanaweza na wako tayari kutoa mchango zaidi katika sekta ya TEHAMA nchini na kimataifa kwa ujumla."

Shindano la TEHAMA Huawei 2021 lilijumuisha zaidi ya nchi 80 ulimwenguni, likiwa na washiriki 150,000 kutoka zaidi ya vyuo vikuu na vyuo vikuu 2,000. Shindano hilo lilizinduliwa katika kanda ya Afrika miaka sita tu iliyopita.

ama
ALHAMISI MACHI 24, 2022
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

Bingwa wa tiba achambua mabinti wadogo wanavyonasa saratani uzazi



Ukurasa 13

Serikali yaamka kujihami na ujio wa homa manjano jirani



Ukurasa 14

Manispaa Kahama na 'operesheni nawa mikono' kabla Uviko hadi 2025

KERO NDANI YA AFYA

# Viongozi wa SHIVYAWATA wapaza sauti yanayowasibu wenye ulemavu

**Na Beatrice Philemon**

NI miaka mingi wenye ulemavu wamekwamishwa katika upatikanaji wa haki zao nyingi za kibinadamu. Hata hivyo, kadri muda unavyoenda kunashuhudiwa mwamko, mabadiliko yake yanashuhudiwa kwamba si kwa asilimia zote.

Kwa kurejea Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu ya Mwaka 2004, inaueleza ulemavu unatokana na dosari mwilini ,akilini au vyote kwa pamoja.

Hiyo humsababishia mtu kushindwa kutenda mambo ambayo kwa kawaida angetarajiwa kuyafanya, ulemavu ukibaki kizuizi kwake.

Pia, inafafanua asilimia kubwa ya wananchi wanaopata ulemavu, sababu kuu iko katika afya, umaskini, mazingira, lishe, watoto kukosa chanjo muhimu kwa magonjwa yanayoleta maradhi na matunzo ya kila siku.

Kwa wajawazito au matatizo wakati wa kujifungua, nayo yanachangia kadhia hiyo kwa mama mwenyewe au mtoto atakayezaliwa, hivyo kupatikana huduma za ushauri na matibabu kunachangia kupunguza madhara.

Aidha, kuna eneo la umasikini kwa wenye ulemavu, hata familia zao huwakwaza kupata nyenzo za kujimudu kufikia vituo vya afya kirahisi. Vyote hivyo, vinatajwa kuwafanya hasa walio vijijini washindwe kufika kwenye huduma za afya.

Umoja wa Mataifa mwaka 1948, ulipitisha azimio linaloeleza binadamu wote wamezaliwa sawa na huru na wana haki za kustahili heshima, hali kadhalika naye anawajibika kwa jamii hiyo.



Jamii ya wenye ulemavu katika moja ya mjumuiko wao. **PICHA: MTANDAO**

Hapo kuna haki za kuitumia jamii na rasilimali zake kwa ajili ya maendeleo na usalama wake. Hiyo inamfanya mwenye ulemavu kuwa na haki zote za kibinadamu.

**SAUTI YA SHIVYAWATA**

Mweka Hazina wa Jumuiya ya Wanawake na Watoto ya (SHIVYAWATA), Christina Silas, anaiambia Nipashe kwamba kinamama wengi wenye ulemavu wanakumbana na shida nyingi, wanapohitaji huduma za mama na mtoto kwenye vituo vya afya, ikiwamo lugha isiyo rafiki ya watoa huduma.

Pia, analalamika vitanda vya kujifungulia sehemu nyingi bado siyo rafiki, akivieleza 'ni virefu sana' akiendelea: "Unakuta mama mjamzito mwenye ulemavu akienda kujifungua, anapata shida sana hospitali, pia wananyanyapaliwa na watoa huduma."

Christina ambaye pia ni mwanamama, anasisitiza mama hao wanapaswa kupatiwa huduma rafiki na siyo kunyanyapaliwa.

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inasisitiza kwamba binadamu wote ni sawa na wanastahili kupata haki sawa bila kujali rangi, kabila, jinsia na dini zao.

Christina ana ombi: "Serikali iangalie eneo hili, ikiwezekana wanawake wenye ulemavu wanapokwenda kujifungua waruhusiwe kuingia na wasaidizi wa kutafsiri lugha kwenye wodi za kujifungulia, kwa sababu watoa huduma wengine hawana ujuzi..."

Pia, anaomba wasaidiwe vitanda maalumu vinavyowawezesha wajawazito wenye ulemavu kupata huduma sahihi bila ya vikwazo.

Kiongozi huyo wa walemavu ana hoja nyingine: "Unajua hata wanawake wenye ulemavu wana uwezo wa kufanya kazi kama watu wengine wasio na ulemavu, kwa sababu kuna wengine wamesoma hadi ngazi ya chuo kikuu."

Anasema wameshaomba kuanzishwa programu maalum ya kuwajengea uwezo kinamama na wasichana wenye ulemavu kwa jamii zinazowazunguka, ili wamudu kuzijua na kudai haki zao.

Inaelezwa, kumekuwapo tatizo sugu kwa kinamama, wasichana na watoto wenye ulemavu kukosa mifumo ya kutoa taarifa, hata wakafuatilia haki zao zitendeke.

Christina anaongeza kuwa hata mifumo michache iliyopo inakosa weledi, akifafanua: "Wanawake tumekuwa tukinyanyasika kutoka taasisi za wenye ulemavu kwa kutopatiwa nafasi sawa."

**MWENYEKITI WAO**

Mwenyekiti wa SHIVYAWATA, Nuru Awadhi, anaomba msukumo kutoka serikalini na taasisi binafsi ili wenye ulemavu wawezeshwe na kufanyike mabadiliko kisheria kuwalinda wanawake na hasa wenye ulemavu.

Lingine analoliomba ni kuridhiwa Mkataba wa Afrika wa Watu Wenye Ulemavu wa Mwaka 2018, unaoanisha haki za wanawake wenye ulemavu, pia akitaka kuwapo siku ya wanawake wenye ulemavu nchini.

Lingine analolitaja ni kuimarishwa mifumo iliyoanzishwa kama madawati ya jinsia yawe na wataalamu wenye ujuzi wa masuala hayo, katika mustakabali mpana.

**ANENAYO KATIBU**

Katibu wa SHIVYAWATA, Maria Chale, anakiri kuwa sasa watu wengi wameelewa dhana ya watu wenye ualbino, hata wazazi na ndugu wanawalinda sana watoto wenye hali hiyo, tofauti na miaka iliyopita.

"Matokeo ya mauji ya albino asilimia kubwa ni ndugu, lakini kama mzazi akijua kuwa mtoto mwenye ualbino ana haki ya kuishi atalinda usalama wa mtoto wake," anasema.

AFYA

# Bingwa wa tiba achambua mabinti wadogo wanavyonasa saratani



Wasichana wakipata huduma za kitabibu, ikiwamo uangalizi dhidi ya saratani ya shingo ya kizazi, katika moja ya nchi jirani. **PICHA: JARIDA LA UN**

**Na Beatrice Shayo**

"Kuna binti wa miaka 21 alikuja kwangu, baada ya vipimo akawa na saratani ya shingo ya kizazi, nilishtuka sikutaka ajue kama nimeshtuka, ikabidi nimuulize vizuri kaupataje huo ugonjwa kumbe alianza mapenzi akiwa darasa la kwanza na baba yake mdogo."

Ni maneno ya Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Wanawake katika Hospitali ya Muhimbili (MNH), Matilda Ngavina, katika mafunzo kwa wanawake katika Hospitali ya Massana, jijini Dar es Salaam, kuwajengea uwezo umuhimu wa kuchunguza afya, hasa saratani ya shingo ya kizazi na matiti.

"Nilijiuliza huyu binti kaipataje hii saratani ya shingo ya kizazi?" Dk. Matilda, anadokeza.

"Akanisimulia baba yake mdogo alianza naye ngono akiwa darasa la kwanza na kuendelea naye hadi alivyofika darasa la tano. Akagundua hiki kitendo sio kizuri na kumueleza mama yake na kuanza kufuatilia, japo ulitokea mtafaruku mkubwa," anafafanua.

Anaendelea kwa kuasa: "Tunapoishi na watoto wetu tujitahidi kuwalinda na kuwasimamia ili wasije kuanza mapenzi katika umri mdogo bila kuwalinda tutajikuta watoto wetu wanapata saratani ya shingo ya kizazi katika umri mdogo. Hili ni jambo muhimu wazazi walizingatie,"

Tabibu huyo, ambaye ni Rais wa Chama cha Madaktari Bingwa Afrika Mashariki, anasema zamani wenye saratani ya shingo ya kizazi wengi walikuwa katika umri kuanzia miaka 50, ikilinganishwa na sasa mabinti wanabainika kuanza ngono katika umri mdogo.

> **Hizo ni dalili muhimu ambazo mtu anatakiwa kuzifuatilia na kwa wale ambao wameshapoteza siku zao wanapata dalili ya kuanza kuona damu utakapoona dalili hizo ni muhimu kuwahi kituo cha afya na kufanya uchunguzi.**



Rais wa Chama cha Madaktari Bingwa Afrika Mashariki, Matilda Ngavina. **PICHA: BEATRICE SHAYO**

### WAHOFIA MIONZI

Dk. Matilda anasema kuna changamoto za baadhi ya wagonjwa wenye saratani wanaposikia suala la kupigwa mionzi, wanatafuta mbadala wa mitishamba ambayo ni hatari kwa usalama wa afya zao.

Anafafanua, sababu kuu ni kukosa uelewa na kwamba wanaposikia mionzi, wanafananisha na jua linalowachoma usoni na kubabuka, jambo ambalo si la kweli.

"Kuna hili jambo la watu kuogopa mionzi pale mgonjwa, anapojulishwa katika matibabu anatafuta njia mbadala ambayo kwake, anaona anaiweza kuimudu kuliko hii ambayo wanamuambia, hii ndio shida ambayo tunaipata," anasema.

Anasema, mgonjwa anatumia mitishamba badala ya mionzi na anapozidiwa, akifikishwa hospitali yupo katika hali mbaya kutokana na kukaidi maagizo aliyopatiwa.

Dk. Matilda anataja tatizo lingine analokutana nalo ni namna wanavyotibu wagonjwa wa saratani ya shingo ya kizazi na wengi hawana uelewa wa mzizi wa ugonjwa wenyewe, ulivyokaa mwilini, watu wanachelewa kufika katika vituo vya afya kutibiwa.

"Tunapata wagonjwa ambao wamefikia hatua mbaya ya ugonjwa, hali ambayo naweza kumsaidia mgonjwa ni kupata mionzi. Watu hawana uelewa wa kufanya uchunguzi mapema kama inavyotakiwa, huu ugonjwa ungepungua na kuondoka," anasema.

Anasimulia: "Wengi wao ni waoga kufanya kipimo utamsikia mtu ananimbia Dk. Ngavina kweli nikuvulie nguo yangu ya ndani? Nitakuja siku nyingine kufanya hicho kipimo."

Hapo anashauri: " Sijaona cha kuogopa, jambo la muhimu ni kutakiwa kujua usalama wa afya yako mapema badala ya kuchelewa,".

Anaeleza namna Watanzania wangezingatia uchunguzi mapema, ingewasaidia kujua katika hatua za awali, kabla ya kubadilika kufikia hali kamili ya saratani, kwani ugonjwa unatibika pale mtu anapowahi kugundua.

"Saratani ya hatua ya kwanza inatibika bila shida, watu wengi wanaogopa mionzi, wanaogopa dawa za saratani, kwa hiyo wanaishia kufa kwa sababu ya kutokutibiwa kwa ajili ya hofu ya ugonjwa," anasema.

Aidha, anasema kwa Hospitali ya Muhimbuli kuna kinamama katika wodi zenye magonjwa ya saratani na Hospitali ya Ocean Road, jijini Dar es Salaam, wana wagonjwa wa saratani ya shingo ya kizazi.

"Ni saratani ya shingo ya kizazi naweza kusema inayoongoza kwa kuwadhuru Watanzania. Hivyo, kuna haja ya kutoa elimu kwa wingi ili wajitokeze katika kufanya vipimo mapema, badala ya kuchelewa. Unakuja kuambiwa ugonjwa upo katika hatua mbaya ambayo huwezi kupona,"anasema.

### SABABU & DALILI

Daktari huyo anasema chanzo cha ugonjwa wa saratani ya kizazi, ni maambukizi ya kirusi anachokitaja kwa jina lake Human Papilloma Virus (HPV), ambao unapatikana kwa kufanya mapenzi katika umri mdogo.

"Hiki kirusi kinatoka kwa mwanaume ambaye anaingia kwako kupitia tendo la ndoa. Sio kila tendo la ndoa linaambukiza na sio kila ukifanya tendo la ndoa unapata saratani ya shingo ya kizazi," anafafanua.

Anataja dalili muhimu za kuzingatiwa, ni kutokwa damu kwenye utaratibu usioeleweka, kutokwa damu wakati wa kujamiana, kutokwa maji yanayonuka ukeni.

"Hizo ni dalili muhimu ambazo mtu anatakiwa kuzifuatilia na kwa wale ambao wameshapoteza siku zao wanapata dalili ya kuanza kuona damu utakapoona dalili hizo ni muhimu kuwahi kituo cha afya na kufanya uchunguzi," anasema.

### USHAURI KWA MABINTI

Dk. Matilda anaweka tahadhari kwamba anayeanza ngono kuanzia miaka 10 na zaidi anatakiwa kwenda kwa daktari na kumtaarifu ili afanyiwe uchunguzi wa saratani ya shingo ya kizazi na akibainika kuwapo shida anapelekwa katika hatua inayofuata.

"Hilo ni muhimu kuzingatia na mabinti zetu tuwapatie chanjo zinazotolewa kuanzia umri wa miaka 11 hadi miaka 16 zinafanya kazi akishatumia hiyo chanjo anakuwa salama," anasema Dk. Matilda

AFYA

## TANGU ITOWEKE ZAMA 1950...

# Serikali yaamka kujihami na ujio wa homa manjano kutoka jirani

• WHO yafunda mbinu za kudhibiti janga nchini

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

BAADA ya kutokea mlipuko wa homa ya manjano nchi jirani ya Kenya kulikoripotiwa hivi karibuni, Shirika la Afya Duniani (WHO) na serikali kwa pamoja zimeanza kuchukua hatua za tahadhari.

Hiyo inajumuisha kupiga marufuku watu kutoka mataifa yenye tishio la ugonjwa huo, kuingia nchini bila ya kuwa na cheti kinachothibitishwa kuchanja.

Aidha, watumishi wa afya mipakani wametakiwa kuacha kujihusisha na vitendo vya udanganyifu wa kutoa vyeti kwa watu ambao hawajachanja chanjo ya homa ya manjano.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu amebainisha hayo alipokua akizungumza na waandishi wa habari kuhusu tahadhari ya mlipuko wa homa ya manjano kwa wananchi, akiwa na ufafanuzi:

"Mnamo Machi 3, 2022 Wizara ya Afya ilipokea taarifa kutoka Ofisi ya Shirika la Afya Duniani (WHO) iliyopo hapa nchini, ikielezea kuwepo kwa mlipuko wa ugonjwa wa homa ya manjano nchini Kenya katika Kaunti ya Isiolo, umbali wa takribani kilomita 285 Kaskazini mwa Nairobi.

"Taarifa hiyo ilieleza kuwa, mgonjwa wa kwanza mwenye dalili za ugonjwa huu alipatikana mnamo tarehe 12 Januari 2022 na hadi kufikia tarehe 3 Machi 2022, kulikuwa na jumla ya wagonjwa 15 na vifo vitatu vilivyotokana na ugonjwa huo."

Aidha, anasema kati ya sampuli sita zilizopimwa katika maabara ya Kenya (KEMRI), tatu zilithibitika kuwa na virusi vya homa ya manjano na taarifa hiyo ya WHO, inasema kumekuwapo tetesi za wagonjwa wenye dalili za homa ya manjano katika nchi za Uganda, Sudan ya Kusini na Chad.

"Hapa nchini kwetu taarifa za kipindi cha miezi mitatu iliyopita katika mfumo wa ufuatiliaji wa magonjwa yaliyopewa kipaumbelewa zinaonyesha kuwa hapakuwepo na taarifa zinazoashiria kuwepo ugonjwa wa homa ya manjano.

"Vilevile, katika kipindi hiki mfumo wa taarifa wa ufuatiliaji wa tetesi za magonjwa haujaashiria kuwepo kwa dalili za ugonjwa huo hapa nchini. Hata hivyo, ninatoa tahadhari kwa wananchi ili kuchukua hatua na kuhakikisha ugonjwa huu hauingii nchini kwetu" anasisitiza Waziri Ummy.

Anasema baada ya kupata taarifa hizo za ugonjwa nchini Kenya, serikali kupitia Wizara ya Afya inaendelea kuchukua hatua stahiki, ikiwamo kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji watu wenye dalili za ugonjwa huo katika vituo vya afya bandarini, viwanja vya ndege na mipakani kwa wasafiri watokao nje ya nchi.



Mganga Mkuu wa Serikali Dk. Aifello Sichalwe, akiwa jijini Dodoma anaelezea tahadhari ya mlipuko wa ugonjwa wa homa ya manjano katika nchi jirani ya Kenya. **PICHA ZOTE: MTANDAO**



Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, akizungumza kwenye tukio hilo.

Pia, anasema serikali inahakikisha wasafiri watokao nchi zenye hatari ya ugonjwa huo, wanakuwa na uthibitisho wa chanjo ya homa ya manjano, kabla ya kuruhusiwa kuingia nchini.

"Wizara itaendelea kufanya yafuatayo kufuatilia kwa karibu wasafiri wote wanaoingia nchini, hususani kutoka nchi zilizo hatarini kuambukizwa homa ya manjano, kuhakikisha chanjo za kutosha za ugonjwa wa homa ya manjano zinakuwepo nchini, kusimamia na kuhimiza usafi wa mazingira ili kudhibiti mazalia ya mbu, kuendelea kutoa elimu ya afya kwa wananchi kuhusu ugonjwa huu" anasisitiza Waziri Ummy.

Waziri anasema, wizara anayotumikia sasa inawaasa wananchi kutoa taarifa mapema katika vituo vya kutoa huduma za afya, wanapomuona mgonjwa mwenye dalili zinazofanana na ugonjwa huo.

"Kutumia vyandarua vilivyotiwa dawa kutilia mkazo usafi wa mazingira na kuzuia maji yasituame ovyo kwenye mazingira tunayoishi, ili kuangamiza mazalia ya mbu katika maeneo yetu," anafafanua

### HATUA ZA KINGA

Kwa wasafiri wanaoenda nje ya nchi, anawataka wahakikishe wanapata chanjo dhidi ya homa ya manjano na anaongeza kuwa huduma za chanjo zinapatikana katika Uwanja wa Ndege wa Mwalimu Nyerere (Dar es Salaam), Hospitali ya Mnazi Mmoja, bandarini (Dar es Salaam) na Kituo cha Afya cha IST (Dar es Salaam) pamoja na ofisi za afya zilizoko mipakani.

Rais anawataka Watanzania kuwa watulivu na kusikiliza maelekezo na ushauri utakaotolewa na wataalam wa afya, katika maeneo yao au vyombo vya habari.

Vilevile, Waziri Ummy, ameagiza Mganga Mkuu wa Serikali kuhakikisha huduma za chanjo ya homa za manjano zinatolewa katika hospitali zote za rufani za mikoa kuanzia sasa.

### MWAKILISHI WHO

Mwakilishi Mkazi wa WHO nchini, Dk. Tigest Mangestu, anaeleza homa ya manjano inasababishwa na virusi vinavyoenezwa na mbu aina ya andes, kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu, vilevile kati ya binadamu wenyewe.

Anasema watu wanaofanya kazi kwenye misitu, huweza kuambukizwa kwa kung'atwa na mbu hata wakapata vimelea vya ugonjwa huo kutoka kwa wanyama kama nyani porini.

Vilevile, anaeleza ugonjwa huo huambukizwa kati ya mtu, pindi mtu mwenye virusi hivyo anapoumwa na mbu na hatimaye kueneza kwa mtu mwingine.

"Dalili za ugonjwa wa homa ya manjano ni pamoja na homa, kuumwa na kichwa, maumivu ya misuli pamoja na mgongo, mwili kutetemeka, kupoteza hamu ya kula, kusikia kichefuchefu," anafafanua:

Dk. Mangestu anaendelea: "Pia kutapika, mwili kuwa na manjano kutokwa na damu sehemu za wazi kama mdomoni, puani, machoni na tumboni na wakati mwingine damu huonekana kwenye matapishi na kinyesi na ugonjwa unapokuwa mkali figo hushindwa kufanya kazi."

> Serikali inahakikisha wasafiri watokao nchi zenye hatari ya ugonjwa huo, wanakuwa na uthibitisho wa chanjo ya homa ya manjano, kabla ya kuruhusiwa kuingia nchini.

Anaainisha kuwa kipindi cha kuonekana kwa dalili za ugonjwa huo, ni kati ya siku tatu hadi sita baada ya kuambukizwa. Mwakilishi huyo anasema, homa ya manjano haina tiba maalum na mgonjwa anayezidiwa huhitaji huduma ya karibu na anatibiwa kulingana na dalili zinazojitokeza.

Lingine analolitaja, ni mara nyingi matibabu yao huhusisha utoaji dawa za kushusha homa, kupunguza maumivu au kuongezewa maji mwilini au kwa kuwekewa dripu.

Anaueleza ugonjwa huo unaozuilika kwa chanjo na Shirika la Afya Duniani (WHO), anasema chanjo hutolewa kwa wasafiri hasa wanaokwenda katika nchi zenye ugonjwa huo, ili kuwadhibiti dhidi ya maambukizi wasiugue au hata kuja nayo pindi wanaporejea.

Anasema, pamoja na utoaji wa chanjo hiyo kwa wasafiri, umekuwa ukifanyika mipakani, ili kuhakikisha wasafiri wanaoingia kutoka katika nchi zenye ugonjwa huo, wawe na vyeti stahiki vinavyothibitisha wamechanjwa.

Anasema, katika nchi za Afrika Mashariki, Tanzania haijawahi kuwa na taarifa ya mgonjwa aliyethibitika kuwa na homa ya manjano tangu mwaka 1950.

Wito wake ni kwa wadau katika ngazi zote, waendelee kushirikiana kutekeleza jitihada za kupambana na magonjwa ya milipuko, ikiwamo homa ya manjano, kwa kuzingatia miongozo inayotolewa na wizara husika.

AFYA

# Manispaa Kahama na 'operesheni nawa mikono' ya 2016 hadi 2025

• Wenyeji wakiri wameumwa sana kwa uchafu



Abiria katika kituo kidogo cha Mabasi akinawa mikono kwa sabuni na maji tiririka kabla ya kuingia ndani ya basi kuanza safari..
**PICHA: MTANDAO**

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

KUNAWA mikono kwa sabuni na maji tiririka mara kwa mara ni njia mojawapo muhimu sana katika mapambano dhidi ya maradhi ya kuambukiza yatokanayo na uchafu, ikiwamo kichocho pamoja na kuhara damu na mpya wa Uviko 19.

Aidha, kutokana na umuhimu wa unawaji wa mikono salama, Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO) kwa kushirikiana na wadau wa afya, walianzisha siku maalumu ya kunawa mikono duniani inayoadhimishwa kila mwaka mwezi Oktoba, lengo ni kuhamasisha jamii unawaji mikono.

Kunawa mikono ni utaratibu maalumu wa kutumia maji safi yenye kutiririka na sabuni kwa kufuata hatua maalumu, kwa muda usiopungua sekunde 20 na umekuwa ukifanywa zaidi na watu wanaoishi mjini. ukilinganishwa na wale wanaoishi pembezoni.

Maradhi mengi yanayozikumba jamii zetu yanatokana na tabia ya kutonawa mikono ipasavyo ni kipindupindu, kuharisha, kuhara damu, minyoo, kope, malaria na maradhi ya mifumo ya kupumua ikiwamo ugonjwa ulioikumba duniani mwaka 2019 Covid-19.

Unawaji wa mikono hufanyika kabla na baada ya kushika au kula chakula kinachohitaji mikono kutumika, baada ya kutoka chooni, kushika mnyama au kinyesi chochote kile ama cha binadamu au mnyama na kumsafisha mtoto aliyejisaidia ni muhimu kunawa.

Pia, inahusu kabla ya kutayarisha chakula, kushika taka zikiwamo zile za kufagia au kufanya shughuli yeyote ile ya usafi.

> "Niwe mkweli sikuwahi kuwa na desturi ya kunawa mikono wakati wa maandalizi ya chakula na hii sio kwangu tu ni kwa watu wote.

### KINACHOJIRI KAHAMA

Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, iko katika Kampeni ya Usafi wa Mazingira iliyozinduliwa tangu mwaka 2016 na inakoma 2025, ikilenga kutatua changamoto za usafi wa mazingira.

Ofisa Afya wa Manispaa hiyo Basil Gerivas, anasema, kabla ya ujio wa ugonjwa wa Uviko-19 hali ya magonjwa yatokanayo na uchafu yalikuwa yamekithiri hasa kwa wanaoishi pembezoni na asilimia kubwa walikuwa watoto.

### HALI YA MLIPUKO

Basil anasema kabla ya ujio wa Uviko-19, hali ya magonjwa ya mlipuko ilishika kasi, wananchi wakiripotiwa kuugua kila mara, walikuwa zaidi ni watoto wadogo na wanawake, hasa wanaoishi pembezoni mwa mji.

Anaeleza takwimu mwaka 2019 wagonjwa wa kuhara kawaida walikuwa 50,101 hao ni wanaofika katika vituo vya afya kupata huduma, mwaka 2020 wagonjwa walikuwa 46,502 huku mwaka jana 30,912.

Basili anatoa takwimu ya mfano, mwaka 2019 waliogundulika kuwa na ugonjwa wa minyoo walikuwa 11,637, huku mwaka 2020 walikuwa 10,198, na mwaka jana wagonjwa 7,224, vilevile anasema wagonjwa waligundulika kuwa na upungufu wa maji yaani kutokana na kuhara.

Anasema kupungua magonjwa hayo, kunatokana na elimu ambayo wamekuwa wakitoa kila mara katika maeneo ya mikusanyiko, kuhusu taratibu za kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni wakati wote, hata na wakati mwingine kabla ya kutayarisha chakula na baada.

### VYOO BORA

Basil anasema suala la ukosefu wa vyoo bora katika kaya linasababisha wananchi kuendelea kupata magonjwa hayo yatokanayo na usafi na wamekuwa wakiendelea kuwasisitiza wananchi juu ya umuhimu wa kujenga vyoo bora kwa ajili ya afya zao kwa kuweka maji ya kunawa mikono baada ya kutoka chooni.

Anasema Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, ina zaidi ya kaya 49,000 kwa mujibu wa Sensa ya Makazi ya Mwaka 2012 na kwa kushirikiana na wenyeviti wa mitaa, watendaji wa kata na maofisa afya, wanaendelea kuwahamasisha wananchi kujenga vyoo katika magulio, minada na maeneo ya biashara zao.

Basili anasema kabla ya kuzindua kampeni ya 'Nyumba ni Choo' hali ya ujenzi wa vyoo bora Manispaa ya Kahama' ilikuwa mbaya na kila mtu alikuwa akijenga choo ili mradi kujisitiri, ila baada ya kampeni hiyo na kuweka mikakati ya kuwatoza faini wasiokuwa na vyoo, sasa wamebadilika.

Anataja takwimu ya mwaka 2019, Manispaa nzima ya Kahama, ilikuwa na vyoo bora 35,806 sawa na asilimia 75.2, idadi ambayo ni ndogo ikilinganishwa na idadi ya kaya zilizopo na mwaka 2020 vyoo bora viliongezeka na kufikia vyoo 45,847 sawa na asilimia 76.9.

Basil anasema utoaji elimu na faini kwa kaya zisizokuwa na huduma ya choo umesababisha kuongezeka kwa vyoo bora na mwaka jana 2021 kulikuwa na vyoo bora 46,096 sawa na asilimia 78.2, wakaidi walifikishwa mahakamani.

### FAINI & CHANGAMOTO.

Basili anasema, wakati wa uzinduzi wa kampeni ya usafi wa mazingira mkoani Shinyanga chini ya aliyekuwa Mkuu wa mkoa Zainabu Telack waliweka mikakati ya kuwatoza faini ya kiasi cha Sh.500,000 kwa kata itayakosa huduma ya choo bora baada ya kupeana muda wa kujenga vyoo hivyo.

Anasema tangu mwaka 2019 mpaka sasa, wametoza faini za jumla ya Sh. milioni 19.7 kaya zisizokuwa na vyoo na baadhi yao kuwafikisha mahakamani kwa kushindwa kabisa kujenga vyoo na utozaji wa faini hizo ni makubaliano baina yao na serikali na zoezi la kuwapiga faini linaendelea kwa wale wanaoshindwa kufuata maelekezo.

"Tunawatoza faini kwa mujibu wa sheria ndogo za Halmashauri yetu kiwango cha chini ni Sh.200,000 na kwa anayekaidi kufuata maelekezo tunamtoza zaidi au kumfikisha mahakamani na faini hizo zinawagusa pia wanaotiririsha majitaka wakati wa mvua za masika," anasema Basili.

Hata hivyo anasema hali ya kiuchumi inasababisha baadhi ya wananchi kushindwa kujenga vyoo bora vinavyohitajika na badala yake wanajenga vyoo vya kujisitiri tu na ndiyo maana wanakwenda nao polepole katika kuwapatia elimu ili kuendelea kupambana na kuhakikisha ifikapo mwaka 2025 kaya zote zinakuwa na vyoo bora.

### WANANCHI MANISPAA

Erick Godfrey, mkazi wa Nyandekwa anasema awali kabla ya kupata elimu ya umuhimu wa choo bora, alikuwa na choo cha kawaida na kwa kuwa anaishi pembezoni mwa mji aliona hakuna maana ya kujenga choo kinachokidhi mahitaji na matakwa ya watu wa afya.

Anasema familia yake ilikuwa kubwa na magonjwa ya mlipuko yatokanayo na uchafu, kila wiki alipata mgonjwa nyumbani kwake. Baada ya kupata ushauri hali iliboreka, kutokana na mabadiliko aliyofanya hakuna tena magonjwa hayo.

Sarah George anasema, kuibuka janga la Uviko-19 kumewafanya kujenga desturi ya kunawa mikono mara kwa mara tofauti na awali kwani hata yeye alikuwa miongoni mwa waliokuwa hawanawi mikoni wanapofanya shughuli zao za maandalizi ya chakula.

"Niwe mkweli sikuwahi kuwa na desturi ya kunawa mikono wakati wa maandalizi ya chakula na hii sio kwangu tu ni kwa watu wote" anafafanua.



## Sababu ugonjwa wa macho Bahi yatajwa

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

IMEELEZWA kuwa chanzo cha ugonjwa wa macho kwa wakazi wa Bahi mkoani Dodoma ni uwapo wa nzi wadogo kwenye maeneo hayo wanaoathiri mtoto wa jicho. Kutokana na hali hiyo, Mbunge wa Bahi, Kenneth Nollo, kwa kushirikiana na Ubalozi wa Qatar nchini Tanzania, wameweka kambi ya matibabu ya macho wilayani humo.

Daktari Bingwa wa Macho kutoka Hospitali ya Macho Mvumi mkoani hapo, Dk. Andrew Kirumbi, aliyasema hayo jana kwenye ufunguzi wa kambi hiyo kwa wananchi wa Tarafa ya Mundemu wilayani humo.

"Chanzo cha ugonjwa wa macho hapa Bahi unasababishwa na aina ya nzi wadogo walioko kwenye maeneo haya ambao wanasababisha mtoto wa jicho kufa," alisema.

Alibainisha kuwa ubalozi unasaidia vipimo na matibabu kwa wananchi kwenye kambi hiyo iliyowekwa baadhi ya maeneo wilayani humo.

Kadhalika, alisema madaktari bingwa kutoka Hospitali ya Mvumi na Hospitali ya Tumbi mkoani Pwani wako katika kambi hizo ili kusaidia matibabu hayo. "Kwa siku ya kwanza wananchi 286 walijitokeza kupima macho katika Kituo cha Afya cha Mundemu na walioonekana na tatizo na watafanyiwa upasuaji, matarajio yetu ni kuwafikia wananchi wengi zaidi wenye matatizo haya," alisema.

Naye Nollo, alisema aliomba ufadhili wa matibabu hayo kutoka ubalozi huo ili kusaidia wananchi wengi wa jimbo hilo.

Nollo alisema awamu ya kwanza wananchi 806 walipatiwa matibabu kwenye Tarafa ya Mwitikira na kati ya hao 146 walifanyiwa upasuaji. Alisema ametoa Sh. milioni 14 ili kufanikisha matibabu hayo kwa wananchi wake.

Mkurungenzi wa Shirika la Qatar Charity na Mwakilishi wa Balozi Qatar nchini Tanzania, Ahmed Elhamrawy, alisema baada ya ombi la mbunge huyo waliona wafike kusaidia matibabu hayo.

Elhamrawy alisema pamoja na matibabu hayo wananchi watakaobainika kuwa tatizo na kufanyiwa upasuaji taasisi hiyo itawapatia miwani bure.

Alisema taasisi hiyo inasaidia sekta ya afya kwa kujenga zahanati na vituo vya afya kwenye jamaii kutokana na bajeti waliopanga.

Aliyataja maeneo mengine wanayosaidia kuwa ni matibabu ya macho pamoja na huduma mbalimbali za kiafya kwa wananchi na kwamba kwa sasa sasa taasisi hiyo inaendelea na huduma za kiafya kwenye maeneo nane hapa nchini ambapo walianzia na Hospitali ya Tumbi.

Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Mwanahamisi Munkunda, aliwashukuru ubalozi huo kwa msaada huo na kuwahimiza wananchi wenye matatizo ya macho kuchangamkia fursa hiyo inayozunguka kwenye tarafa zao.

# Ndalichako aonya watumishi wa umma wanaoendekeza rushwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, amesema hatamvumilia mtumishi yeyote atakayejihusisha na rushwa katika utoaji huduma.

Licha ya kutoa onyo hilo, Ndalichako amesisitiza uadilifu kwenye vibali vya kazi kwa raia wa kigeni.

Prof. Ndalichako aliyasema hayo jana jijini hapo alipokuwa akizindua Baraza la Kwanza la Wafanyakazi wa Ofisi hiyo ambalo pamoja na mambo mengine, lina jukumu la kupokea na kujadili bajeti ya wizara kwa mwaka 2022/23 na utekelezaji wa bajeti ya mwaka ulioisha.

"Suala la rushwa na ubadhirifu wa mali za umma niseme mtu anayetaka kujua rangi yangu halisi, achezee fedha za wizara au ajihusishe na masuala ya rushwa. Kamwe hatutakuwa na uvumilivu na mtumishi atakayejihusisha na masuala ya rushwa kwa kuwa kazi tunazofanya zina ushawishi.

"Unaenda kumkagua mtu ambaye hazingatii sheria za kazi, ni tajiri na mwekezaji mkubwa ni rahisi sana kusema usiandike ripoti nitakukatia chochote.

"Unaandaa mafao mtu ana kitita kikubwa wewe mfukoni huna kitu unamwandikia hundi unamwambia utanipa kiasi gani. Unatengeneza mazingira ya kuchelewesha kwa makusudi. Niwasihi sana kujiepusha na rushwa, kitu kidogo kinakuondolea utu, usikubaali kuuza utu wako," alisema.

Prof. Ndalichako alisema uwapo wa mfumo wa utoaji vibali umepunguza mlologo na urasimu na kuwataka kuwafuatilia ili kuhakikisha mfumo unafanya kazi vizuri na unatoa vibali kwa wakati.

"Nitoe wito kwa wanaofanya kazi ya utoaji vibali kuhakikisha hakuna mianya yoyote ya rushwa katika utoaji wa vibali mahali pa kazi," alisema.

Aliwataka viongozi na watumishi katika ofisi hiyo kuzingatia weledi, nidhamu na maadili ya utumishi wa umma ili kutoa huduma bora kwa wananchi.

Wajibu wa kila mtumishi, alisema ni kufanya kazi kwa bidii na nidhamu ya hali ya juu huku akisisitiza uwapo wa mabaraza ya wafanyakazi katika maeneo ya kazi ambayo yamekuwa chachu ya kuongeza ufanisi na tija kwa wafanyakazi kwa kusaidia kuimarisha ushirikiano baina ya wafanyakazi na waajiri ili kutekeleza majukumu yao kwa weledi.

Alimwagiza Kamishna wa Kazi kukagua muda wa kuingia na kutoka kazini kwa wafanyakazi wa wizara hiyo baada ya kubaini wengine hawazingatii muda uliopangwa na serikali.

Mwenyekiti wa Baraza la Chama cha Wafanyakazi wa Serikali Kuu na Afya (TUGHE), Tawi la Ofisi hiyo, Godfrey Chacha, alisema baraza pamoja na majukumu mengine, lina kazi ya kupanga mipango na kushauri viongozi na watumishi kuhusu ufanisi wa kazi na hatua zinazotakiwa kuchukuliwa ili kuhakikisha huduma zinatolewa kwa wakati na kwa ubora unaokubalika ili kufanya kazi kwa uadilifu.



Mkuu wa Wilaya ya Bahi mkoani Dodoma, Mwanahamisi Mukunda (kulia), akizungumza na Mwakilishi wa Ubalozi wa Qatar hapa nchini ambaye ni Mkurugenzi wa Shirika la Qatar Charity, Ahmed Elhamrawy (kushoto), walipokutana kwenye zoezi la upimaji macho kwa wananchi katika Kijiji cha Mundemu wilayani humo juzi. Katikati ni Mbunge wa Jimbo la Bahi, Keneth Nollo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wanawake UCSAF wawakumbuka wagonjwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WANAWAKE wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF), wametoa msaada wa vyakula mbalimbali na taulo za kike kwa wagonjwa wa afya ya akili katika Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe huku wakitoa wito kwa jamii na taasisi zingine kuwasaidia wagonjwa hao.

Akikabidhi msaada huo jana wenye thamani ya Sh. milioni 3.5, Ofisa Mtendaji Mkuu wa UCSAF, Justina Mashiba, alisema wanawake hao wametoa msaada huo ikiwa ni sehemu ya kuadhimisha mwezi wa wanawake duniani.

"Tumekuja kutoa msaada hapa Mirembe na kuwasalimia wagonjwa kama njia mojawapo ya kurudisha tulichojaliwa kwa jamii hasa ukizingatia Machi ni mwezi wa wanawake.

Natoa wito kwa jamii na taasisi zingine tuwasaidie ndugu zetu waliopo hospitalini hapa wanaopata matibabu wana mahitaji mengi hospitali pekee haiwezi kuwatimizia," alisema.

Naye Mkurugenzi Mtendaji Hospitali hiyo, Dk. Paul Lawala, alisema msaada uliotolewa ni muhimu kwao kwa kundi hilo la wagonjwa.

Kwa upande wake, Katibu wa Afya wa Hospitali hiyo, Jackson Mjinja, aliishukuru UCSAF kwa kuwapelekea matendo hayo ya huruma na kuomba na watu wengine waguswe kupeleka misaada kama hiyo kwa kuwa wagonjwa wenye matatizo ya afya ya akili wana mahitaji mengi kama watu wengine.

Alibainisha kuwa hospitali inahudumia wagonjwa wa akili na wenye kesi 234, walioathirika na dawa za kulevya 524.

Pia alisema kuna watu sita kwenye eneo la kilimo na ufugaji Hombolo ambao wametelekezwa na jamii.

"Tunatoa shukrani UCSAF kwa ushirikiano mzuri ulioko hadi kuwiwa kuleta msaada huu," alisema.





# Zaidi ya watoto 200,000 kuchanjwa chanjo polio

**Na Grace Mwakalinga,** SONGWE

ZAIDI ya watoto 200,000 wenye umri chini ya miaka mitano, mkoani Songwe wanatarajia kupata chanjo ya ugonjwa wa polio lengo likiwa ni kuwakinga na ugonjwa huo ambao tayari umekwisha ripotiwa nchi jirani ya Malawi.

Akizungumza na Nipashe jana, Mratibu wa chanjo Mkoa wa Songwe, Moses Lyimo, alisema uchanjani unaanza leo hadi Machi 27 na chanjo zitatolewa kwa watoto wote wa mkoa huo.

Alisema uchanjaji utaendeshwa na watoa huduma 1,874 ambao watafika nyumba kwa nyumba kuchanja watoto wote wenye umri chini ya miaka mitano.

"Maandalizi yote yamekamilika tuna vifaa vya kutosha, wataalamu wa afya kuanzia ngazi ya kata hadi wilaya wamepata mafunzo kuhusu uchanjaji pamoja na kutoa elimu kwa wazazi na walezi na kuonyesha utayari wa kufanikisha zoezi hilo," alisema Lyimo.

Alisema jumla ya watoto 33,589 wa Wilaya ya Songwe watapata chanjo ya polio, Mbozi, watoto 97,460, Ileje 23,107, Tunduma 29,606 na Momba 45,696.

Aliongeza kuwa kila halmashauri imeunda timu ya watu watatu kutoa huduma hiyo na atakuwapo mtoa chanjo, anayechanja na atakayekuwa anachukua rekodi ya zoezi hilo.

Alisema uchanjaji utaendeshwa nyumba kwa nyumba, maeneo ya shule pamoja na vituo vya afya huku kamati za afya kuanzia ngazi ya wilaya na mkoa zikisimamia.

"Ili kufanikisha zoezi hilo kwa Mkoa wa Songwe, watoa huduma wa chanjo watawekewa alama ya tiki kwa kutumia chaki katika kila nyumba itakayofikiwa na zoezi hilo, huku watoto watakaochanjwa kuwekewa wino kwenye kidole ambao utakaa ndani ya wiki mbili wino huo utasaidia kufanya utambuzi wa watoto waliopata chanjo," alisema Lyimo.

Alisema baada ya kukamilika kwa siku nne imeandaliwa timu itakayopita nyumba kwa nyumba ili kuhakiki na kujiridhisha watoto waliopata chanjo.

Baadhi ya wakazi wa Wilaya ya Mbozi, akiwamo Mesia Sichawe, aliupongeza uongozi wa Mkoa wa Songwe kuanza utoaji wa chanjo hiyo kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano na kwamba wako tayari kutoa ushirikiano.

Sichawe alisema baada ya kupata taarifa za uwepo wa ugonjwa nchini Malawi kupitia vyombo vya habari waliingia hofu na kuiomba serikali kujipanga kikamilifu kudhibiti maambukizi ya ugonjwa huo mkoani Songwe.




Meneja wa Taasisi ya Tulia Trust, Jacqueline Boaz (kushoto), akikabidhi cheti cha kutambua mchango wa gazeti la Nipashe katika kufanikisha Tamasha la Ngoma za Jadi 2021 kwa mwakilishi wa gazeti hilo, Nebart Msokwa, jijini Mbeya juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## Kamati ya Bunge yaridhishwa ujenzi sekondari

**Na Grace Mwakalinga,** RUNGWE

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa, imeeleza kuridhishwa na kasi ya ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya shule ya sekondari kongwe nchini ya wavulana Rungwe baada ya majengo ya shule hiyo kuchakaa.

Hayo yalisemwa jana na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Boniface Butondo, ambao walifanya ziara ya kukagua maendeleo ya uboreshaji wa miundombinu ya sekondari hiyo.

Alisema mradi huo utasaidia kwa wanafunzi kusoma kwa bidii na kupata mafanikio ikiwamo kuongeza ufaulu kwa wanafunzi.

"Serikali yetu inaendelea kufanya mambo makubwa katika uboreshaji na ujenzi wa vyumba vya madarasa kote nchini, Shule ya Sekondari Rungwe ni miongoni mwa wanufaika, wanapongeza wasimamizi wa mradi huu wa ukarabati miundombinu kwa sababu kazi imeonekana muhimu ni wanafunzi wetu kusoma kwa bidii ili kutimiza ndoto zao," alisema Butondo.

Vile vile, alilishukuru Baraza la Madiwani pamoja na uongozi wa wilaya kwa kusimamia na kufuatilia kwa ukaribu ukarabati wa shule hiyo kongwe nchini ambapo baada ya kubana matumizi ya fedha pia walijenga bweni lingine la wanafunzi.

Alisema shule hiyo ilianza mwaka 1961 na ukarabati ulianza mwaka 2020 na kukamilika mapema mwaka huu.

Alisema jumla ya Sh. milioni 172 zilitumika kukarabati miundombinu ya shule hiyo ikiwamo vyumba vya madarasa, mabweni pamoja na jengo la utawala.

Shule ya Sekondari ya Wavulana Rungwe ina jumla ya wanafunzi 400 kati yao wapo wanaosoma masomo mbalimbali ya sayansi na biashara.

# Wawili washikiliwa tuhuma za mauaji

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi mkoani Songwe, linawashikilia watu wawili kwa makosa mawili tofauti ya mauaji likiwamo la mmoja kumuua mkewe kwa kumtwanga na kitu kizito kwenye paji la uso.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na wandishi wa habari kuhusu udhibiti wa matukio ya uhalifu mkoani humo.

Katika tukio la kwanza Kamanda Matei alisema Machi 20 majira ya saa saba mchana jeshi hilo lilifanya msako katika Kijiji cha Chitete, Kata ya Iwindi, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya na kumkamata mtuhumiwa Safari Luwole (43), mkazi wa Horongo ambaye alikuwa akitafutwa kwa kosa la mauaji ya mke wake Tumain Anthon (45), aliyeuawa Febrauri 4, mwaka huu.

Kamanda Matei alisema, Februari 4, mwaka huu majira ya saa moja asubuhi katika kijiji cha Inolo wilayani Mbeya, Tumain Anthon, alikutwa ndani ya nyumba yake akiwa amefariki dunia baada ya kupigwa na kitu kizito kwenye paji la uso na mume wake, Safari Luwale.

Matei alisema baada ya kufanya msako huo wa kumkamata mtuhumiwa walibaini chanzo cha mauaji hayo ni ugomvi wa kifamilia kati ya marehemu na mumewe.

Aliongeza kuwa baada ya kupata taarifa za mauaji hayo Jeshi la Polisi lilianza msako na Machi 20, walimkamata mtuhumiwa na upelelezi wa shauri hilo unaendelea ili mtuhumiwa atafikishwa mahakamani kujibu shtaka hilo.

Katika tukio lingine la mauaji ni kwamba Jeshi la Polisi Mbeya na Songwe lilifanya msako na Machi 21, majira ya saa 11 jioni katika Kijiji cha Mwak- Tunduma mkoani Songwe walimkamata mtuhumiwa Emmanuel Patsonmwesa (22), ambaye alikuwa akitafutwa kwa kosa la mauaji ya bosi wake, Asumwisye Lufingo (37), wilayani Chunya aliyeuawa Januari 2, mwaka huu akiwa shambani kwake.

Matei alisema Lufingo aliuawa kwa kukatwa na mapanga maeneo ya kichwani na mwili wake, tukio hilo alilifanya akishirikiana na mwenzake.

Alisema chanzo cha mauaji hayo ni madai ya fedha ya ujira ya kulima shamba na baada ya kutekeleza tukio hilo watuhumiwa waliondoka na pikipiki ya marehemu yenye namba za usajili MC.776 BES aina ya Fekon.

"Aidha Jeshi la Polisi mkoani hapa linaendelea na msako wa kumtafuta mtuhumiwa mwingine ambaye walishirikiana katika tukio hili, lakini mahojiano na mtuhumiwa yanaendelea ili kubaini ilipo pikipiki ya marehemu waliyoondoka nayo baada ya kufanya tukio hilo," alisema Kamanda Matei.





## Zantel inavyothamini mchango wa w/'biashara

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

KAMPUNI ya simu za mkononi Zantel kupitia huduma ya lipia kwa simu imesema inathamini mchango wa wafanyabiashara wanaotumia huduma hiyo na kurahisisha kutotembea na fedha nyingi mfukoni.

Kauli hiyo ilitolewa na Mtaalamu wa Huduma ya Ezy Pesa wa Zantel, Eunice Hubert Alelyo, wakati akizungumza katika mkutano wa wafanyabiashara mbalimbali wanaotumia huduma ya lipia kwa simu, Kiembesamaki.

Alisema huduma hiyo ina faida kubwa hasa uhifadhi na usalama wa fedha za mfanyabiashara hivyo ni vyema kuitumia ili kukuza soko la fedha na kumrahisishia mteja kuitumia muda wowote anapohitaji bidhaa.

Aidha, alisema lengo kubwa la mkutano huo ni kutoa elimu kwa wafanyabiashara wanaotumia huduma ya lipia kwa simu ambao bado hawajajua umuhimu na faida ya huduma hiyo.

Eunice alibainisha kwamba huduma hiyo inawahusu zaidi wafanyabiashara wa Zanzibar wanaotoa huduma mbalimbali za kibiashara ikiwamo nguo, mikahawa na inamsaidia mfanyabiashara kukusanya mapato yake kwa urahisi.

Alibainisha kuwa kampuni hiyo imekuwa ikiboresha huduma mbalimbali ili kuwawezesha wananchi kupata huduma hizo kwa urahisi na huduma nyengine muhimu ikiwamo internet.

Hata hivyo, akizungumzia lengo la mkutano huo alisema ni kuwaelimisha wafayabiashara na kuongeza ujuzi katika kutanua biashara zao na kwenda kidijitali katika kutumia mfumo huo wa lipia kwa simu.

Alisema hadi sasa wana wafanyabiashara zaidi ya 4,000 hasa katika maeneo ya mjini ambao wameipokea huduma hiyo, lakini kwa upande wa Pemba katika maeneo ya Wete na Chakechake pia wameipokea kwa mwamko mkubwa.

Eunice aliwataka wafanyabiashara kuwa mabalozi wazuri wa kutoa elimu kwa wateja wanaofika kupata bidhaa mbalimbali wanazohitaji wakiwa kwenye maduka yao.

Sambamba na hayo alisema huduma hiyo itapunguza tatizo la wizi wa kimtandao na haina gharama za tozo kwa wanaotumia huduma ya lipa kwa simu.

Naye Yassir Baharudin, mtaalamu wa teknolojia ya mtandao alisema kutokana na kukua kwa huduma ya mawasiliano ya kimtandao ni vyema kwa wananchi kuwa na mfumo wa huduma ya lipia kwa simu ili kurahisisha ununuzi wanapokuwa njiani na sio kutegemea kutoa pesa kwa mawakala.

Kwa upande wao wafanyabiashara wanaotoa huduma kupitia mtandao walisema huduma hiyo kwa kiasi kikubwa inarahisisha utoaji wa huduma kwa wateja wao.

# Rais Mwinyi atoa pole Kaskazini Unguja

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ametuma salamu za pole kwa wananchi waliopatwa na maafa kutokana na upepo mkali uliotokea huko katika vijiji vya Kendwa na Nungwi Mkoa wa Kaskazini Unguja. Katika salamu hizo, Dk. Mwinyi alisema kuwa serikali yake kupitia Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa Zanzibar iliyoko katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais itafanya tathmini tukio hilo ili kujua hasara halisi iliyojitokeza ili kuwafariji wananchi waliofikwa na maafa hayo.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayoub Mohammed Mahmoud, upepo mkali ulitokea katika vijiji vya Kendwa na Nungwi Shehia ya Kiungani, Mkoa wa Kaskazini Unguja na kusababisha maafa kwa nyumba zipatazo 36.

Pia upepo huo uliotokea juzi majira ya saa 5:00 asubuhi ulisababisha uharibifu katika sehemu za majengo ya hoteli tatu za kitalii kwenye mkoa huo ambapo hakuna mwananchi aliyefariki kutokana na tukio hilo. Rais Dk. Mwinyi amewasihi na kuwaombea kwa mwenyezi Mungu wananchi wote waliopatwa na maafa hayo kuwa na subira katika kipindi hiki kigumu.

Katika hatua nyingine, Shekha wa Shehia ya Kendwa, Omar Khamis, alisema familia saba zimekosa makazi kabisa kutokana na upepo huo uliosababisha nyumba 36 kuezuka paa.

"Familia hizo ilibidi zisadiwe kwa ajili ya makazi kwa sababu nyumba zao hazikaliki kabisa," alisema Shekha huyo.

Aidha, aliwataka wananchi kuchukua tahadhari katika kipindi hichi cha mvua za masika zilizoanza kunyesha ambazo zimeambatana na upepo.



Waziri Ofisi ya Rais Zanzibar anayeshughulikia Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrick Soraga (kushoto), akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa Smile Communication Tanzania, Zuweina Farah, baada ya kuzindua mtandao wa kasi wa Smile 4G LTE na bidhaa zake, jijini Zanzibar juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Makamu wa Rais asisitiza umuhimu wa vyuo vikuu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema kuwapo kwa vyuo vikuu ni muhimu katika kutekeleza utafiti ili kusaidia mipango ya maendeleo itakayochangia kukuza uchumi wa nchi.

Othman aliyasema hayo jana, katika ziara yake inayoendelea visiwani akitembelea taasisi za sekta ya elimu, binafsi na za serikali, zikiwamo vyuo vikuu.

Akiongea kwa nyakati tofauti, alisema thamani ya vyuo vikuu inaonekana pale taasisi hizo zinapojikita katika kutekeleza tafiti mbalimbali, ambazo hatimaye husaidia kutoa miongozo juu ya utatuzi wa changamoto zinazoikabili jamii na nchi kwa ujumla.

Othman alishauri vyuo vikuu kuwa wabunifu ili kwenda sambamba na mabadiliko ya sasa duniani, yakiwamo ya elimu na teknolojia, na yatakayowezesha taasisi hizo kujiwekea mtaji na kujiendesha hali itakayoepusha utegemezi wa moja kwa moja serikalini.

Akisisitiza umuhimu wa kuzitathmini shule za asili, Othman alisema, "ili kuinua kiwango cha elimu kitakacholeta maendeleo ni vyema kuvienzi vituo vyetu hivi ambavyo vinaweza kuwa ni uwekezaji muhimu ambapo pia nchi inaweza kuneemeka."

Aidha, alitilia mkazo umuhimu wa kuwekeza katika lugha ya Kiswahili na zile za kigeni, ndani ya taasisi za elimu, akisisitiza kuwa hiyo itaweza kukuza mawasiliano, hasa kwa wawekezaji kwa kuzingatia pia mfumo wa uchumi wa huduma (Service Oriented Economy) kwa Zanzibar.

Naye Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Leila Mohamed Mussa, alieleza kuwa serikali imeshazibaini changamoto zinazokabili taasisi na sekta ya elimu kwa ujumla hivyo kinachohitajika ni kujenga ushirikiano ili kusaidia utatuzi wake.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Rashid Hadidi Rashid amepongeza mashirikiano na juhudi zinazochukuliwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, zikiwamo kasi ya ujenzi wa shule hiyo maalum.

Katika ziara hiyo, Othman ametembelea taasisi mbalimbali za elimu ambazo ni pamoja na Shule ya Sekondari ya Lumumba, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Vyuo Vikuu vya Zanzibar (ZU) na Abdulrahman Alsumeit (Sumeit University), na baadaye kukagua Maendeleo ya Ujenzi wa Skuli ya Mjumuisho ya Jendele, Wilaya ya Kati, Mkoa wa Kusini Unguja.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**ANTAR SAID MBARAK** anatangaza kupotelewa kwa kadi ya aina ya GARI (ISUZU) yenye namba za usajili **T 434 CKT, CHASSIS NO:710258988.** yeyote atakaeiyona atoe taarifa kituo cha polisi au piga simu namba **0714540452**

POLISI TAARIFA:
**MOR/MOR/RB/118635/2022**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**ANYEGILE ANDENDEKISYE MWAMALUKA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **MITSUBISH FUSO** yenye **NAMBA YA USAJILI T.692 CSF** rangi ya bluu. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.

TAARIFA POLISI:
**MBE/MBE/RB//116083202**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**

**WILAYA YA MOROGORO**
**LILILOPO MOROGORO**

**MAOMBI MADOGO NAMBA 32 YA 2022**

**GERALD MISINZO..................................MUOMBAJI**

**DHIDI YA**

**JULIANA JERRY ARMSTRONG.......... MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA**

**JULIANA JERRY ARMSTRONG** popote ulipo unaarifiwa ufike katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Morogoro tarehe 25/4/2022 mbele ya Mwenyekiti E.Mogasa wewe mwenyewe binafsi au utume muwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa.
Endapo hautahudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi

Imetolewa kwa MKONO wangu na MUHURI Baraza leo tarehe 23 Mwezi Machi,2022.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
MOROGORO.

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**JANETH JOACHIM SOKA** anatangaza kupotelewa kwa kadi ya aina ya **SUBARU IMPREZZA** yenye namba za usajili **T 982 DCG.** yeyote atakaeiyona atoe taarifa kituo cha polisi.

POLISI TAARIFA:
**DAR/URA/RB/116935/2022**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo Kihonda**

**Wilaya ya Morogoro**

**Mkoa Wa Morogoro**

**Usimamizi wa Mirathi......21..2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU SHABAN H MHANDO WA M/SONGO KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA SAIDI IDDI KINYOGOLI**

**TANGAZO**

**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 24/03 /2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Endapo kuna yoyote mwenye wosia na marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia ya narehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika.

Imetolewa Tarehe 17/03/2022

HAKIMU

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo Wilaya ya IRINGA**

**Kituo cha BOMANI Mkoa IRINGA**

**Usimazi wa mirathi Na 43 /2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU SHAHMIRY ABDULNABII BIHROM**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA 43/2022**

**TANGAZO**

***(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)***

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowowte/madlahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 20 Mwezi 4 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimazi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

* Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa.
* Marehemu hakuacha wosia.
* Futa isiyohusika.

Imetolewa leo Tarehe 21 Mwezii 3 Mwaka 2022

.............................................
HAKIMU
RESIDENT MAGISTRATE
IRINGA

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**KAHAMA IMPORT AND EXPORT LTD** anatangaza kupotelewa na kadi ya Bajaji yenye **NAMBA ZA USAJILI T.911CWT** yenye **CHASSIS NO. L3YHDLZC5EBL00024, Engine No. 164MLEFL00024** yenye radi nyekundu. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake.

Taarifa ya polisi:
**KAH/ TR/RB/175/2022.**


***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 0782253676**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## SIKU 28; MASHAMBULIZI RUSSIA - UKRAINE



Bendi ya Lviv National Philharmonic ikifanya onyesho la burudani mubashara, kwenye mji wa Lviv, ambao haujaguswa na mapigano na kwa wengi waliokimbia makazi yao, kituo chao cha kwanza ndani ya Ukraine ni Lviv, katika mji huo uliopo Magharibi wenye urithi wa utamaduni. **PICHA: AP**

# NATO kuijadili Russia, Ukraine

**Brussels,** UBELGIJI

JUMUIYA ya Kujihami (NATO) inakutana mjini Brussels pamoja na ajenda nyingine inatarajiwa kutangaza duru mpya ya vikwazo dhidi ya Russia kwa uvamizi wake nchini Ukraine.

Rais wa Marekani, Joe Biden pia ameelekea Brussels, Ubelgiji, ambako atakutana na viongozi wa muungano wa kijeshi wa NATO na washirika wa Ulaya.

Mshauri wa Usalama wa kitaifa wa White House, Jake Sullivan, aliwaambia waandishi wa habari: Ataungana na washirika wetu katika kuweka vikwazo zaidi kwa Russia na kuimarisha vikwazo vilivyoko ili kukabiliana na ukwepaji na kuhakikisha utekelezwaji thabiti."

Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelenskyy, anatarajiwa kuhutubia kwa njia ya video mkutano mkuu wa NATO Alhamisi, na alisema kabla ya mkutano huo kwamba anatarajia viongozi wa nchi za Magharibi kuongeza vikwazo vyao dhidi ya Russia na kuahidi msaada zaidi kwa Ukraine.

Takriban mwezi mmoja baada ya vikosi vya Russia kuivamia Ukraine, kuna ishara zinazoongezeka kwamba vikosi vya Ukraine vina ujasiri mkubwa, vikilenga wanajeshi wa Russia na wakati mwingine, kuchukua udhibiti wa maeneo yaliyokuwa yametwaliwa na Russia.

Wizara ya Ulinzi ya Ukraine ilisema juzi kwamba vikosi vyake vimechukua tena Makariv, kitongoji cha mji mkuu wa Kyiv, kufuatia mapigano makali.

Wanajeshi wa Ukraine pia wameonekana kuanzisha mashambulizi katika mji wa Mashariki wa Izyum, kilomita 120 Kusini Mashariki mwa Kharkiv, na katika maeneo ya karibu na mji wa Kherson, Kusini mwa nchi hiyo.

Akitoka Ubelgiji, Biden anatarajiwa kufanya ziara nchini Poland.

> Russia ndiyo inayoongoza duniani katika makombora ya hypersonic, ambayo kasi yake inafanya kuwa vigumu kuidungua.

**RAMAPHOSA AILAUMU NATO**

Wachambuzi wa maasuala ya siasa wanasema, Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa amepunguza ushawishi wake kama mpatanishi wa mgogoro wa vita nchini Ukraine, akiwa na pendekezo lenye utata kwamba hatua za NATO ndizo za kulaumiwa kwa uvamizi wa Russia dhidi ya jirani yake wa Magharibi.

Ramaphosa anasema anapendelea mazungumzo badala ya silaha au vikwazo vya kiuchumi akimaanisha vikwazo vilivyowekwa dhidi ya Russia kutoka Marekani na washirika wa Magharibi baada ya uvamizi huo, ambao sasa ni wiki yake ya nne.

Vita hivyo vingeepukika kama NATO ingezingatia maonyo kutoka kwa viongozi na maofisa wake kwa miaka mingi, kwamba upanuzi wake wa mashariki ungesababisha kukosekana kwa utulivu katika eneo hilo, Ramaphosa aliliambia bunge, Alhamisi wiki iliyopita.

Aliongeza kuwa Afrika Kusini, haiwezi kuunga mkono matumizi ya nguvu, na ukiukaji wa sheria za kimataifa.

Rais wa Afrika Kusini, amesema nchi yake iliombwa kuwa mpatanishi katika mzozo huo, lakini hakumtaja ni nani aliyeiomba Afrika Kusini kuingilia kati.

**RUSSIA YAONYA**

Msemaji wa Kremlin, Dmitry Peskov amesema katika mahojiano kwamba Russia itatumia tu silaha za nyuklia ikiwa kuwepo kwake kutatishiwa.

Maoni ya Peskov yalikuja akihojiwa na kituo cha CNN na aliyasema wakati mtangazaji Christiane Amanpour alipomuuliza iwapo "ameshawishika au anajiamini" kwamba Rais Vladimir Putin hatatumia chaguo la nyuklia katika vita vya Ukraine.

"Tuna sera ya usalama wa ndani, na ni ya umma. Unaweza kusoma sababu zote za silaha za nyuklia kutumika," Peskov anasema Jumanne.

"Kwa hivyo ikiwa ni tishio linalowezekana kwa nchi yetu, basi inaweza kutumika kwa mujibu wa hali hiyo."

Sambamba na agizo hilo, Wizara ya Ulinzi ya Russia, imesema Februari 28 mwaka huu kwamba, vikosi vyake vya makombora ya nyuklia na meli za Kaskazini na Pasifiki, zimewekwa kwenye hali iliyoimarishwa ya mapigano, shirika la habari la Interfax liliripoti.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Antonio Guterres, amesema kwamba matarajio ya mzozo wa nyuklia, ambayo hapo awali haukuweza kufikiria, sasa yamerudi katika hali inayowezekana.

Peskov pia aliiambia CNN kwamba vita vya Russia nchini Ukraine vilikuwa vinaendelea kulingana na mipango na madhumuni ambayo yalianzishwa hapo awali.

Maoni hayo yanakuja baada ya Rais wa Marekani, Joe Biden kuonya kwamba Putin anafikiria kutumia silaha za kemikali na kibaiolojia nchini Ukraine, huku akieleza mbinu za Moscow kuwa za ukatili.

Wiki iliyopita Russia, ilisema kuwa imerusha kombora lake la hypersonic la Kinzhal (Dagger) ambalo linaweza kulenga shabaha popote pale duniani ndani ya saa moja.

Putin amesema kwamba Russia ndiyo inayoongoza duniani katika makombora ya hypersonic, ambayo kasi yake inafanya kuwa vigumu kuidungua.

Makombora ya Kinzhal ni sehemu ya safu ya silaha iliyozinduliwa mnamo 2018. Urusi ilitumia kombora la hypersonic kwa mara ya kwanza wakati wa kampeni yake ya kijeshi nchini Syria mwaka 2016.

Vita hivyo vimetikisa makubaliano ya usalama wa dunia baada ya vita baridi, kuhatarisha usambazaji wa mazao muhimu duniani na kuibua wasiwasi kwamba kunaweza kuanzisha ajali ya nyuklia.

Kando, moto wa mwituni ulizuka karibu na kinu cha nyuklia cha Chernobyl kilichoacha kutumiwa Ukraine, Waziri wa Maliasili wa nchi hiyo, amesema kuwa miale hiyo imezimwa na mionzi ilikuwa ndani ya viwango vya kawaida.

Chernobyl, mwaka 1986 ilikuwa eneo la msiba mbaya zaidi wa nyuklia duniani.

***Imeandaliwa na Christina Mwakangale kwa msaada wa mtandao***

# JKU WAIHOFIA MACHOMANE MBIO ZA LIGI KUU Z'BAR LEO

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WAKATI Ligi Kuu Zanzibar raundi ya 24 ikitarajiwa kuendelea leo, Alhamisi kwa kupigwa mechi mbili, Kocha wa Maafande wa JKU, Sheha Khamis, amesema licha ya wapinzani wao, Machomane kuwa nafasi ya pili kutoka mkiani, kamwe hawezi kuwachukulia poa, kwa kuwa timu zinazoshika nafasi za chini huwa hazitabiriki kwenye mechi za mwishoni mwa msimu.

Maafande wa JKU wataikaribisha timu ya Machomane kutoka Pemba katika mchezo huo wa Ligi Kuu utakaopigwa katika Uwanja wa Amaan leo.

Machomane wanashuka dimbani wakiwa nafasi ya pili kutoka mkiani na alama zao tisa wakati wenyeji wao JKU wakiwa nafasi ya pili kutoka kileleni baada ya kuvuna alama 44 hadi sasa kwenye mechi 23 walizocheza.

Mechi nyingine itakayopigwa leo itakuwa kati ya Maafande wa KVZ ambao wataikaribisha timu ya Yosso Boys katika Uwanja wa Gombani Kisiwani Pemba.

Timu ya KVZ inashuka dimbani ikiwa na alama 41 kwenye nafasi ya nne katika msimamo wa ligi hiyo huku timu ya Yosso Boys ikiwa katika mstari wa hatari wa kushuka daraja baada ya kukusanya alama 12 zilizotokana na michezo 23, hivyo kushika nafasi ya 14 kati ya timu 18 zinazoshiriki Ligi Kuu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha wa JKU, Sheha Khamis, alisema lengo lake anataka kuhakikisha anashinda michezo zote saba iliyobakia katika mzunguko huu wa lala salama.

Alisema kamwe hawezi kukata tamaa ya kutwaa ubingwa licha ya aliyejuu yao katika msimamo wa ligi kutofautiana naye kwa alama 10, kwani anaamini kwenye soka lolote linaweza kutokea.

Alisema katika michezo hii iliyobakia ataendelea kucheza kwa ushindani zaidi ili kuhakikisha lengo lao la kushinda mechi zote saba za mwisho linatimia.

Akizungumza kuhusu wapinzani wao, Machomane ambao wanaelekea kushuka daraja kutokana na nafasi waliyoko kwenye msimamo wa ligi hiyo, alisema timu zilizo katika nafasi ya mwisho huwa zinacheza kwa kujituma zaidi ili kuhakikisha zinapata matokeo mazuri.

"Sisi malengo yetu ni alama tatu, lakini na wapinzani wetu pia wanazihitaji, lolote linaweza kutokea kwa sababu michezo ya mwishoni mwa ligi siku zote huwa migumu.

Ligi Kuu ya Zanzibar inaelekea ukingoni mwa msimu huu wa 2021/22 huku bodi ya ligi ikitarajia kukutana na klabu shiriki kujadiliana kwa pamoja kuhusu kuendelea kucheza ndani ya Mwezi wa Ramadhani ama kusitisha hadi upite.

**TUNAJIFUA...**



Wachezaji wa timu ya Taifa ya Tanzania, 'Taifa Stars', Zawadi Mauya (kushoto) na Mbwana Samatta, wakiwa mazoezini katika Uwanja wa JMK Park jijini Dar es Salaam juzi kujiandaa na michezo mitatu ya kirafiki dhidi ya Jamhuri ya Afrika ya Kati (uliopigwa jana usiku katika Uwanja wa Benjamin Mkapa), Botswana na Sudan. Kulia ni Kocha Msaidizi wa Stars, Shadrack Nsajigwa. **PICHA: TFF**

# Azam, Dodoma Jiji zala kibano TFF

**Na Adam Fungamwango**

BODI ya Ligi nchini (TPLB), imezipigwa faini Klabu ya Azam FC na Dodoma Jiji kutokana na makosa ya kukiuka kanuni kwenye mechi zao zilizopita za raundi ya 18 ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Wakati Dodoma Jiji ikipigwa faini ya Sh. 500,000, Azam FC imepigwa faini ya shilingi milioni moja, baada ya Kamati ya Uendeshaji na Usimamizi wa Bodi ya Ligi Tanzania Bara kukaa na kupitia mwenendo na matukio mbalimbali ya ligi.

Taarifa iliyotolewa na kamati hiyo iliyokaa Jumatatu wiki hii, ni kwamba timu ya Dodoma Jiji imetozwa Sh. 500,000 kwa kushindwa kuandaa watu wa huduma ya kwanza kwa ajili ya mchezo namba 140, kati ya timu hiyo na Mbeya Kwanza uliochezwa Machi 13, mwaka huu katika Uwanja wa Jamhuri Dodoma na wenyeji kushinda mabao 2-0.

Taarifa hiyo imeeleza kuwa, kitendo cha kushindwa kuandaa watu wa huduma ya kwanza kilisababisha kamishna wa mchezo huo kuchukua hatua kwa kushirikiana na wasimamizi wa kituo kutafuta watu wa dharura.

Adhabu hiyo ni kwa kuzingatia kanuni ya 17 (48), na 17 (60) ya Ligi Kuu kuhusu taratibu za kimchezo.

Nayo klabu ya Azam imetozwa faini ya shilingi milioni moja, kwa kosa la baadhi ya mashabiki wake kutoa lugha za matusi kwa maofisa wa mchezo namba 143 dhidi ya Namungo uliochezwa Uwanja wa Ilulu mjini Lindi, baada ya kuzuiwa kwenda kwenye chumba cha kubadilishia nguo cha timu yao na maofisa usalama uwanjani hapo.

Kwenye mechi hiyo iliyochezwa Machi 16, mwaka huu, Azam ilishinda mabao 2-1.

Adhabu hiyo ni kwa mujibu wa kanuni ya 47 (1) ya Ligi Kuu kuhusu udhibiti kwa klabu.

# Prisons yamweka pembeni kocha

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Prisons imemweka pembeni kocha wake Msaidizi, Shaaban Kazumba kwa kile kilichoelezwa imempangia kazi nyingine.

Mwenyekiti wa klabu hiyo, Enock Mwanguku, amesema Kazumba amepangiwa majukumu mengine na hayupo kwenye kikosi cha Prisons na hajafukuzwa kama baadhi ya mashabiki wa soka wanavyodhani.

"Kamanda huwa haondoki na wala hafukuzwi, amepangiwa majukumu mengine ya kikazi na hapo anakuja mwingine ili mambo mengine yaendelee, bado ataendelea kutoa ushauri na tutaupokea, lakini kama uongozi umeona ana umuhimu wa kwenda kufanya majukumu mengine ya kikazi," alisema mwenyekiti huyo.

Kulikuwa na tetesi kuwa Kazumba ameondolewa kutokana na ombi la Kocha Mkuu, Patrick Odhiambo, lakini mwenyekiti amepinga hilo.

"Hilo halipo, haya ni masuala ya kikazi na hata huko anakokwenda ana majukumu mazuri zaidi kuliko hata haya," alisema.

Kuhusu matokeo mabaya ya Prisons, amesema wameshalijua tatizo na wameanza kulitatua.

"Tumekwisha jitathmini, tutakaa vizuri, shida ipo sehemu moja tu, ni kwamba tunapata matokeo mabaya, lakini tumeshajua tatizo. Ni tatizo la kiufundi ambalo siwezi kulisema kwa sababu tutawapa mbinu wapinzani wetu tutakaocheza nao, mechi zijazo tutakaa vizuri," alisema mwenyekiti huyo.

Prisons inaburuza mkia, ikiwa kwenye nafasi ya 16, ikicheza mechi 18, ikiwa na pointi 13.

Timu hiyo imeshinda mechi tatu na kupata sare nne, ikipoteza mechi 11.

## ZISIKUPITE

### SALAH ATAKIWA JUVE

KLABU ya Juventus wanatayarisha kitita kikubwa cha fedha ili kumnasa mshambuliaji wa Misri mwenye umri wa miaka 29, Mohamed Salah kutoka Liverpool hadi Turin. (***La Gazzetta dello Sport***)

### LOPETEGUI AFIKIRIWA UNITED

MANCHESTER United wanamfikiria kocha wa Sevilla, Julen Lopetegui mwenye umri wa miaka 55, huku wakiendelea kutafuta mrithi wakudumu wa Ralf Rangnick. (***Marca***)

### KESSIE SAFI BARCELONA

KIUNGO wa kati wa Ivory Coast, Franck Kessie mwenye umri wa miaka 25, amefikia makubaliano ya mkataba wa miaka minne na Barcelona na atajiunga na klabu hiyo ya Nou Camp msimu huu wa majira ya joto wakati mkataba wake na AC Milan utakapokamilika. (***Guardian***)

### JOVIC HATAKIWI MADRID

MSHAMBULIAJI wa Serbia, Luka Jovic mwenye umri wa miaka 24, si sehemu ya mpango wa kocha wa Real Madrid, Carlo Ancelotti na pia ataondoka klabuni hapo msimu huu wa majira ya joto. (***Marca***)

### KELLY ATAKIWA NEWCASTLE

KLABU Newcastle wameongeza juhudi za kumsajili beki wa kati wa Bournemouth mwenye umri wa miaka 23, Lloyd Kelly katika mkataba wa pauni milioni 12. (***Express***)

### HAZARD AKERWA MADRID

WINGA wa Ubelgiji, Eden Hazard amechanganyikiwa na kughadhabishwa na Klabu ya Real Madrid, ambayo ina nia ya kumuuza kiungo huyo mwenye umri wa miaka 31 msimu huu wa majira ya joto. (***Goal***)

### RAPHINHA AIKATALIA LEEDS

MSHAMBULIAJI wa Brazil, Raphinha mwenye umri wa miaka 25, amekataa ombi la kwanza la Leeds United kuhusu mkataba mpya. (***UOL***)

### NISTELROOY NA EINDHOVEN

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Manchester United na Uholanzi, Ruudvan Nistelrooy mwenye umri wa miaka 45, anaongoza katika kinyang'anyiro cha kuwa kocha wa PSV Eindhoven. (***Mirror***)

### NEYMAR AMPIKU MESSI

NYOTA wa Brazil, Neymar mwenye umri wa miaka 30, anapokea pauni 600,000 kwa mwezi zaidi ya Muargentina Lionel Messi mwenye miaka 34 katika Klabu ya Paris St-Germain. (***L'Equipe, via Star***)

### ARSENAL YAMTAKA AKTURKOGLU

KLABU ya Arsenal na Tottenham zinamfuatilia winga wa Galatasaray mwenye umri wa miaka 23, Muhammed Kerem Akturkoglu raia wa Uturuki. (***Aksam***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# DEMBELE SASA KUSAINI MKATABA MPYA BARCA

Kama unavyojua, majadiliano hayawezi kuzaa matunda siku moja, lakini Xavi ametuambia...

**BARCELONA,** HISPANIA

OUSMANE Dembele anaweza kusaini mkataba mpya na Barcelona baada ya kuimarika zaidi na zaidi chini ya Kocha Mkuu, Xavi, kwa mujibu wa Makamu wa Rais wa klabu hiyo, Rafa Yuste.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa, Dembele aliarifiwa na Mkurugenzi wa Barca, Mateu Alemany kuondoka klabuni hapo "haraka" wakati wa dirisha dogo la Januari baada ya kuripotiwa kukataa ofa ya mkataba mpya.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, amekuwa akihusishwa na klabu kubwa kwenye madirisha ya uhamisho ya hivi karibuni, lakini kuondoka hapo Camp Nou hakukufanikiwa. Na Dembele sasa amekuwa akitumiwa na Xavi na kuonekana kuwa mchezaji muhimu wa Barca huku majeraha sasa yakionekana kuwa naye mbali.

Awali, ilionekana kama mshambuliaji huyo wa zamani wa Borussia Dortmund angeondoka kwa uhamisho huru mwishoni mwa msimu huu, lakini Yuste ameondoa uwezekano huo.

**"Kama unavyojua, majadiliano hayawezi kuzaa matunda siku moja, lakini Xavi ametuambia ni mchezaji wa aina yake na amechangia mengi kwa klabu," alisema Yuste akiiambia redio Catalunya.**

"Nafikiri Xavi anafanya kazi nzuri, ikiwamo kisaikolojia, kwa sababu Dembele ni mchezaji anayeelewa vizuri mfumo. Iko wazi kwamba Xavi ni kielelezo cha wachezaji.

"Kama atajihisi kuwa bora na bora zaidi, kitu ambacho nafikiri ni kizuri, siwezi kuondoa uwezekano kwamba tunaweza kukutana na wakala wake na kuna uwezekano wa yeye kuendelea kucheza hapa."

Dembele alitengeneza mabao mawili kwa Barcelona kwenye ushindi wa Jumapili wa 4-0 dhidi ya wapinzani wao Real Madrid, wakati Barca wakishinda mchezo wao wa 12 mfululizo kwenye mashindano yote.

Yeye ni mchezaji wa pili wa Barca kutoa asisti mbili kipindi cha kwanza kwenye mchezo wa Clasico katika Uwanja wa Santiago Bernabeu karne hii, baada ya Xavi kufanya hivyo Mei mwaka 2009.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 1,065

MECHI KALI
POTUGAL
VERSUS
TURKEY
1 | 1.37
X | 4.90
2 | 7.99

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588 0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# IBRAHIMOVIC AHOFIA KUSTAAFU SOKA



**STOCKHOLM,** Sweden

MSHAMBULIAJI wa AC Milan na Sweden, Zlatan Ibrahimovic anahofia wazo la kustaafu soka na amesema huenda "akatoweka kabisa" mara tu maisha yake ya uchezaji yatakapokamilika.

Ibrahimovic alifikisha umri wa miaka 40 Oktoba, lakini anabaki kuwa sehemu muhimu ya kikosi cha Milan na anaripotiwa kuwa kwenye mazungumzo ya kusaini mkataba mpya baada ya mwisho wa msimu huu.

Nyota huyo wa zamani wa Barcelona, Paris Saint-Germain na Manchester United amekuwa na majeraha msimu huu, lakini bado ameshiriki mara 22 katika michuano yote akiwa na Milan.

Pamoja na kusaidia kuiongoza Milan mbio za ubingwa wa Ligi Kuu Italia, Scudetto, msimu huu wa kwanza tangu 2011, Ibrahimovic pia anatumaini kuisaidia Sweden kwenye Kombe la Dunia la mwaka huu 2022 baada ya kutengua uamuzi wake wa kustaafu mwaka jana.

Na wakati bado anaitwa kwa klabu na nchi, Ibrahimovic hataki kutundika daluga.

"Nina hofu hii kuhusu kustaafu: nini kitatokea baadaye? Najua nitakuwa na uwezekano wa ofa nyingine," alisema katika mkutano na wanahabari Jumanne akiwa na kikosi cha Sweden.



# *Italia, Argentina kuvaana Wembley*

**NYON,** Uswisi

SHIRIKISHO la Soka la Ulaya, UEFA, limethibitisha kuwa mechi kati ya Italia na Argentina itakaochezwa Jumatano ya Juni Mosi, mwaka huu katika mchezo wa kwanza wa "Finalissima" baada ya miaka 29, utapigwa kwenye Uwanja wa Wembley.

Mechi hiyo ilitangazwa hapo awali Septemba, na uthibitisho Desemba kwamba "Mkataba mpya wa Maelewano (MoU) uliodumu hadi 30 Juni 2028" ulikuwa umetiwa saini kati ya UEFA na CONMEBOL, na kusababisha mchezo kuchezwa London Juni Mosi.

Mchezo huo unawakutanisha washindi wa michuano ya Mataifa ya Ulaya (Euro) na bingwa wa Mataifa ya Amerika Kusini, Copa America.

Marudio ya awali, yakilinganisha mshindi wa mashindano ya hivi majuzi zaidi ya Uropa dhidi ya mshindi wa hivi majuzi zaidi wa Copa America, hapo awali yalijulikana kama Artemio Franchi Trophy na yalifanyika mwaka 1985 na 1993.

Ufaransa iliifunga Ur guay mabao 2-0 kati toleo la kwanza mwa 1985, wakati mchezo 1993 ulishuhudia Argen na wakiongozwa na Die Maradona - wakiifun Denmark kwa mikwaju penalti.

Taarifa kutoka UEFA manne ilithibitisha kwa ba: "Itawapa mashab fursa ya kuwatazar mabingwa wa sasa mabara mawili bora kandanda duniani wa ishiriki, CONMEBOL UEFA.

5,872,000

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 26/03/2022 | 18:00 | AFC Wimbledon vs Cambridge Utd | 2.29 | 3.29 | 2.95 |
| 02. 26/03/2022 | 18:00 | Airdrieonians vs Cove Rangers | 2.73 | 3.27 | 2.42 |
| 03. 26/03/2022 | 18:00 | Elgin City vs Edinburgh City | 2.42 | 3.20 | 2.67 |
| 04. 26/03/2022 | 18:00 | Peterhead vs Falkirk FC | 2.78 | 3.32 | 2.35 |
| 05. 26/03/2022 | 18:00 | Leyton Orient vs Barrow | 2.24 | 3.29 | 3.04 |
| 06. 26/03/2022 | 18:00 | Carlisle vs Bristol Rovers | 2.50 | 3.24 | 2.70 |
| 07. 26/03/2022 | 18:00 | Colchester vs Tranmere | 2.40 | 3.28 | 2.79 |
| 08. 26/03/2022 | 18:00 | Bradford City vs Newport | 2.56 | 3.20 | 2.66 |
| 09. 26/03/2022 | 18:30 | Den Bosch vs VVV Venlo | 2.36 | 3.72 | 2.55 |
| 10. 26/03/2022 | 19:00 | Finland vs Iceland | 2.28 | 3.15 | 3.30 |
| 11. 27/03/2022 | 15:00 | Mirandes vs Ponferradina | 2.31 | 3.14 | 3.04 |
| 12. 27/03/2022 | 17:00 | Burgos vs Tenerife | 3.05 | 3.00 | 2.39 |
| 13. 27/03/2022 | 19:15 | Malaga vs Huesca | 2.49 | 3.08 | 2.83 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMISI - 24/03/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 1212 | South Korea vs Iran | 1.99 | 3.03 | 3.75 |
| 15:00 | 4342 | Lebanon vs Syrian Arab Republic | 2.18 | 2.94 | 3.33 |
| 15:00 | 4550 | Vietnam vs Oman | 2.79 | 3.18 | 2.34 |
| 15:00 | 5559 | Sudeva Delhi FC vs Neroca FC | 3.28 | 3.13 | 2.10 |
| 16:00 | 2549 | PAOK Thessaloniki B vs Pierikos Katerini | 2.05 | 2.84 | 3.85 |
| 16:00 | 2583 | Wigan U23 vs Coventry U23 | 3.66 | 3.95 | 1.74 |
| 16:00 | 2788 | Green Eagles vs Zesco United | 2.55 | 2.69 | 2.98 |
| 16:00 | 5326 | Power Dynamos vs Red Arrows | 2.60 | 2.60 | 3.03 |
| 16:30 | 1079 | PS Tni vs Arema | 3.35 | 2.75 | 2.50 |
| 17:30 | 2028 | Churchill Brothers vs Aizawl FC | 2.64 | 3.12 | 2.50 |
| 17:30 | 3156 | Maccabi Bnot Emek Hefer W vs MS Kiryat Gat W | 5.78 | 4.72 | 1.40 |
| 18:00 | 3557 | China vs Saudi Arabia | 7.73 | 4.06 | 1.38 |
| 18:30 | 5660 | AF Amadou Diallo vs ASEC Mimosas | 7.72 | 3.57 | 1.45 |
| 18:30 | 5973 | Hungary U21 vs San Marino U21 | 1.01 | 19.28 | 67.47 |
| 19:00 | 2603 | Armenia vs Montenegro | 2.69 | 3.24 | 2.64 |
| 19:00 | 4229 | Serbia U21 vs Macedonia U21 | 1.48 | 3.95 | 5.78 |
| 19:30 | 1574 | Israel U21 vs Poland U21 | 2.25 | 3.37 | 2.79 |
| 20:00 | 1949 | Iraq vs United Arab Emirates | 2.45 | 2.94 | 2.84 |
| 20:00 | 2124 | Kosovo vs Burkina Faso | 2.03 | 3.40 | 3.65 |
| 20:00 | 5839 | Moldova vs Kazakhstan | 2.88 | 3.03 | 2.68 |
| 20:00 | 5929 | Estonia vs Cyprus | 2.29 | 3.07 | 3.48 |
| 20:30 | 1420 | Maccabi Kishronot Hadera W vs Hapoel Beer Sheva W | 1.62 | 4.50 | 4.60 |
| 20:35 | 5197 | Hapoel Nir Ramat Hasharon W vs Hapoel Raanana W | 1.71 | 4.06 | 3.72 |
| 21:30 | 3026 | AS Tel Aviv University W vs Hapoel Marmorek Rehovot W | 1.51 | 4.43 | 4.71 |
| 21:30 | 4252 | VfL Alfter vs FC Pesch | 2.65 | 4.04 | 2.11 |
| 21:30 | 4334 | Hungary vs Serbia | 3.56 | 3.20 | 2.14 |
| 21:30 | 5570 | SV Deutz 05 vs Bcv Glesch-Paffendorf | 8.44 | 5.76 | 1.24 |
| 22:30 | 1931 | Encamp vs UE Sant Julia B | 2.51 | 3.86 | 2.26 |
| 22:45 | 1442 | France U21 vs Faroe Islands U21 | 1.01 | 13.52 | 48.29 |
| 22:45 | 1706 | Italy vs North Macedonia | 1.23 | 5.85 | 13.28 |
| 22:45 | 3690 | Portugal vs Turkey | 1.37 | 4.90 | 7.99 |
| 22:45 | 3820 | Sweden vs Czech Republic | 2.04 | 3.20 | 3.90 |
| 22:45 | 4462 | Scotland vs Poland | 2.47 | 3.10 | 3.00 |
| 22:45 | 5121 | Wales vs Austria | 2.75 | 3.06 | 2.70 |

IJUMAA - 25/03/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 02:05 | 2519 | Jamaica vs EL Salvador | 1.90 | 3.17 | 3.85 |
| 02:30 | 1743 | Paraguay vs Ecuador | 3.09 | 2.99 | 2.49 |
| 02:30 | 4871 | Uruguay vs Peru | 1.59 | 3.54 | 6.79 |
| 02:30 | 5446 | Colombia vs Bolivia | 1.10 | 8.98 | 26.93 |
| 02:30 | 5555 | Brazil vs Chile | 1.45 | 4.30 | 7.21 |
| 04:05 | 5012 | Panama vs Honduras | 1.42 | 3.96 | 6.96 |
| 05:00 | 5120 | Mexico vs USA | 1.89 | 3.22 | 3.85 |
| 05:05 | 1865 | Costa Rica vs Canada | 3.03 | 2.89 | 2.36 |
| 14:00 | 4127 | Uganda vs Tajikistan | 2.01 | 3.35 | 3.80 |
| 15:00 | 2593 | Latvia vs Kuwait | 2.27 | 3.31 | 3.16 |
| 20:00 | 4378 | Norway vs Slovakia | 1.76 | 3.44 | 4.99 |
| 21:15 | 1580 | Romania vs Greece | 2.64 | 2.99 | 2.89 |
| 22:15 | 4765 | Luxembourg vs Northern Ireland | 3.31 | 3.21 | 2.24 |
| 22:45 | 5482 | Bosnia and Herzegovina vs Georgia | 1.85 | 3.50 | 4.30 |
| 23:15 | 5974 | France vs Ivory Coast | 1.37 | 4.71 | 8.41 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# GEITA GOLD HAKUNA KUPUMZIKA



**Na Dennis Fussi**

KOCHA wa Geita Gold, Fred Felix Minziro, amesema katika kipindi hiki ambacho Ligi Kuu Tanzania Bara imesimama kupisha michezo ya kimataifa iliyopo kwenye kalenda ya Fifa kwa timu za taifa, hawatapumzika na kwamba wataendelea na mazoezi mwanzo mwisho.

Akizungumza na mwandishi wetu jana, Minziro alisema kikosi chake kinaendelea na mazoezi kama kawaida tangu juzi na wanampango wa kutafuta mechi za kirafiki ikiwamo kukipiga na Pamba au Mbao za Mwanza kabla ya kwenda kuvaana na Mbeya City Aprili 2, mwaka huu.

"Mapumziko ya ligi yaliyopo hatuwezi kuyatumia kwa kupumzika, tangu Jumatatu tunaendelea na mazoezi, mimi nitajiunga kesho (leo Machi 24)," alisema.

"Unajua bado tunahitaji kufanya vizuri, bado tunataka kuondoka hapo tulipo ndiyo maana tunaona mapumziko haya tutumie kujipanga zaidi, hata majeruhi tuliokuwa nao watakuwa wamepona baada ya mapumziko haya na hivyo kuongeza nguvu ndani ya kikosi."



# LaLiga wapania kumulika soka la wanawake nchini

**Na Saada Akida**

SHIRIKISHO la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), limesaini kwa mara nyingine mkataba wa miaka mitatu wa makubaliano na LaLiga kwa lengo la kuleta maendeleo ya soka nchini huku wakati huu likimulika zaidi soka la wanawake , imeelezwa.

Laliga wameongeza mkataba mwingine baada ya mkataba wa awali wa miaka mitatu kumalizika mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Rais wa TFF, Wallace Karia, alisema wameongeza mkataba baada ya ule wa awali kumalizika na kwamba makubalino ya sasa yameenda mbali kwa kuangalia soka la wanawake.

Alisema makubaliano waliyoingia na LaLiga ni kwa manufaa ya klabu za soka nchini, hivyo hazina budi kuitumia fursa vizuri.

"Nasikitika makubaliano ya awali klabu hazikuweza kutumia fursa, isipokuwa Yanga ambao walitumia katika kupata elimu juu ya mchakato wao wa mabadiliko," alisema na aliongeza:

"Safari hii klabu zinatakiwa kuchangamkia fursa ya makubaliano haya kwa sababu ni jambo la msingi kwa maendeleo ya mpira wetu."

Alisema kwa sasa LaLiga wameenda mbali sana katika makubaliano hayo kwa kutoa fursa katika soka la wanawake kwa kutoa elimu pamoja na wachezaji kwenda kufanya majaribio nchini Hispania.

"Ninaamini tukitumia vizuri makubalino haya katika soka la wanawake, tutarajie kuona wachezaji wetu wa kike wakipata nafasi ya kucheza soka la kulipwa nchini Hispania."Pamoja na yote, pia tutaendelea kuwaomba LaLiga pia kuangalia wenzetu katika soka la visiwani Zanzibar," alisema rais huyo wa TFF.

Alisema wako katika mchakato wa kuzungumza na Laliga kuhusu kuandaa semina kwa vyombo vya habari kwa ajili ya kuongeza zaidi taaluma na kufanya kazi kwa weledi mkubwa.

# Michezo

Alhamisi Machi 24, 2022

Nipashe




Dembele sasa kusaini Barca

UKURASA 21

## Azam, Dodoma Jiji, zala kibano TFF

**Na Adam Fungamwango**

BODI ya Ligi nchini (TPLB), imezipigwa faini Klabu ya Azam FC na Dodoma Jiji kutokana na makosa...



HABARI UK. 20

## Ibrahimovic ahofu kupotea akistaafu

**STOCKHOLM,** Sweden

MSHAMBULIAJI wa AC Milan na Sweden, Zlatan Ibrahimovic anahofia wazo la kustaafu soka...



HABARI UK. 22

HIYO...



Luis-Miquissone. **PICHA: MTANDAO**

# Miquissone Simba tena?

## Sinema kama ya Chama yaanza, Al Ahly yatajwa kutaka kumtoa kwa mkopo, Msimbazi wafunguka...

**Na Adam Fungamwango**

KAMA ambavyo zilizuka tetesi za Clatous Chama kurejea Klabu ya Simba kutoka RS Berkane ya Morocco na baadaye ikawa kweli, sinema hiyo imeibuka tena, baada ya kiungo wa zamani wa timu hiyo anayeichezea Al Ahly ya Misri ambao ni Mabingwa wa Afrika, kudaiwa kutaka kurejea tena kwenye klabu hiyo.

**Tetesi za Chama aliyeuzwa RS Berkane Agosti mwaka jana zilianza kama mzaha, lakini zilihitimishwa Desemba alipotangazwa kurejea akiwa ameitumikia timu hiyo kwa miezi minne tu.**

Klabu ya Al Ahly imetajwa kuwa inaweza kumtoa mchezaji wake raia wa Msumbiji, Miquissone kwa mkopo ili kupisha kusajiliwa mchezaji mwingine wa kigeni, huku Simba ikitajwa kupewa kipaumbele.

Vyanzo mbalimbali nchini Misri vinasema kuwa Kocha Mkuu wa Al Ahly, Pitso Mosimane anatarajia kumtoa kwa mkopo kiungo mshambuliaji wake huyo mwenye umri wa miaka 26, msimu ujao kwa madai ya kushindwa kuelewa mfumo wa ufundishaji wake.

Taarifa zimedai kuwa mwenyewe Miquissone anapendelea kurudi klabu yake ya zamani ya Simba iliyomsajili Januari 2020 kipindi cha dirisha dogo kutoka UD Songo alipokuwa akicheza kwa mkopo, akiwa mali ya Mamelodi Sundowns.

Mchezaji huyo aliyesajiliwa na Mabingwa wa Afrika, Al Ahly Agosti mwaka jana akiuzwa pamoja na Chama, amekuwa hana wakati mzuri ndani ya kikosi hicho ambapo licha ya kwamba amekuwa hapati nafasi ya kucheza, lakini baadhi ya mashabiki na wachezaji wa zamani wa klabu hiyo wanadai ni mchezaji mzuri, lakini siyo wa kiwango cha kuichezea timu kama Al Ahly, na alisajiliwa kwa mihemko tu, baada ya kuifunga bao kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa, Februari 23, mwaka jana kati ya mabingwa hao na Simba likiwa pekee kwenye mechi hiyo Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Kama ambayo viongozi wa Simba walivyokuwa wasiri kwenye mkakati wa kumrejesha Chama, wamekuwa wagumu pia kueleza kama wanaweza kumrejesha Miqussone au la kwa mujibu wa taarifa hizo.

Meneja Habari wa Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Ahmed Ally alipoulizwa na Nipashe jana, alisema kuwa bado halijamfikia mezani kwake, na kama lipo basi litakuwa juu kwenye uongozi wa klabu hiyo.

"Sijui kama lipo au halipo, linasikika kwenye tetesi, labda kama lipo basi litakuwa kwenye uongozi wangu wa juu, na kama lipo na likawa tayari kwa kuambiwa wanachama na mashabiki, basi watanipa ili niwahabarishe, lakini kama litakuwa ni tetesi, basi litabaki kama tetesi, ila kwa sasa bado kwangu halijafika," alisema Ahmed.

Viongozi wa Simba kwa miaka ya karibuni wamekuwa wakificha mno mikakati yao hususan ya usajili, kiasi hata suala la Chama lilionekana kama ni tetesi zisizo na mashiko na hekaya za Abunuwasi, lakini lilipofikia tamati likawekwa hadharani.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >